
# Pambazuko

Toleo Namba 156 Jumatatu, Februari 23 - Machi 1, 2026


# Ukata watafuna EAC



- Wabunge wake hawajalipwa tangu Novemba

Habari Uk. 6,&7

Jicho la Tai

## Makonda kaiacha Arusha kuwa uji wa magimbi

HAKIKA uzee una mambo mengi sana. Yaani unaweza kupelekwa huku na kule – ukikwea ndege kwenda mji mmoja hadi mwingine na nchi hii ama ile. Huko haufikishwi kwa ajili ya utalii! La hasha, bali kuisaka tiba.

Safu Uk. 5

## Dkt Nchemba achefukwa madudu serikalini




Habari Uk. 12,&13

## Giza nene utekelezaji Sheria Ununuzi wa Umma

Uk. 15

- Ubungo wajitetea wakidai bajeti ni tatizo

## Pengo kuzikwa kwenye kaburi alilojiandalia



KIFO cha Askofu Mkuu Mstaafu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo kimeacha historia ya mtu aliyekuwa mchungaji mwaminifu, kiongozi mwenye busara... Uk. 20,&21

## ZEC yachoma nyaraka za uchaguzi mkuu

Uk. 25

## Tahariri

# Kongole Dawasa kukumbatia teknolojia

HATUA ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (Dawasa), kuanzisha mfumo wa kidijitali wa kuunganishia wateja huduma ya maji ni mafanikio makubwa yanayostahili pongezi.

Katika zama hizi za mapinduzi ya teknolojia, taasisi za umma zinapochukua hatua za kurahisisha huduma kwa wananchi, zinajenga - siyo tu ufanisi wa kiutendaji, bali pia imani ya umma kwa serikali.

Kwa muda mrefu, wateja waliotaka kuunganishiwa huduma ya maji walilazimika kufika ofisini, kujaza fomu kwa mkono, kusubiri uthibitisho na wakati mwingine kupitia mlolongo mrefu wa taratibu.

Mfumo wa mtandao umeondoa changamoto hizo kwa kuruhusu maombi kufanyika popote na wakati wowote.

Hii ni hatua inayopunguza gharama kwa mteja, kuokoa muda, na kupunguza msongamano katika ofisi za Dawasa.

Zaidi ya hayo, mfumo huu unaongeza uwazi na uwajibikaji. Mteja anaweza kufuatilia hatua ya maombi yake kwa urahisi, jambo linalopunguza mianya ya usumbufu usio wa lazima.

Mabadiliko haya ya kukumbatia usasa yaliyoonyeshwa na Dawasa, ni dalili kuwa taasisi za umma zinaweza kubadilika na kwenda sambamba na mahitaji ya kizazi cha sasa kinachotegemea teknolojia karibu katika kila nyanja ya maisha.

Dar es Salaam ni jiji linalokua kwa kasi, hivyo wakazi wake kuhitaji mifumo bunifu ya utoaji huduma, na siyo kukumbana na usumbufu unaoweza kuepukwa kwa kukumbatia teknolojia – kama walivyofanya Dawasa.

Kuwepo ongezeko kubwa la wakazi wa jiji hilo kubwa na lenye maendeleo ya haraka nchini Tanzania, kunamaanisha uwepo wa mahitaji makubwa ya maji safi na salama tena kwa uhakika, hivyo kwa kurahisisha mchakato wa kuunganishiwa maji, Dawasa imeonyesha uelewa wa changamoto za jiji na dhamira ya kuzikabili kwa mbinu za kisasa zinazobeba urahisi.

Tunatambua kuwa mabadiliko ya kidijitali siyo rahisi; yanahitaji uwekezaji wa miundombinu, mafunzo kwa watumishi na uelimishaji kwa wateja, hivyo Dawasa wanatakiwa sasa “kushikilia” hapohapo kwenye ufanisi mkubwa unaorahisishwa na teknolojia.

Sisi Pambazuko tunaamini hatua hii ni uthibitisho kwamba pale panapokuwa na nia, mafanikio yanawezekana na Dawasa wameweza.

Ni matarajio yetu kuwa mfumo huu utaendelea kuboreshwa, ukijumuisha njia rahisi za malipo, huduma kwa wateja kwa njia ya mtandao, na mifumo ya haraka ya kushughulikia malalamiko.

Kwa kufanya hivi, Dawasa siyo tu imerahisisha huduma ya maji, bali pia imeweka mfano kwa taasisi nyingine za umma nchini ambao unafaa kuigwa ili kuhudumia wananchi kwa haraka na ufanisi.

Walilofanya Dawasa ni taswira ya Tanzania inayojenga uchumi wa kidijitali na kuweka mwananchi katikati ya utoaji huduma.

Hongera Dawasa kwa hatua hii ya kijasiri na ya kimaendeleo, endeleeni kuwa kinara wa mageuzi ya kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa umma.

# Kwa heri Kardinali Pengo



*Makamu wa Rais, Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi akisaini kitabu cha maombolezo ya kifo cha Askofu Mkuu (mstaafu) wa Jimbo Kuu Katoliki Dar es Salaam, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo, alipowasili katika Makazi Kiaskofu ya Jimbo Kuu Katoliki Dar es Salaam, Kurasini kuwasilisha salamu za rambirambi za Rais Samia Suluhu Hassan kufuatia kifo hicho juzi. (Picha na OMR).*


## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**



## TIMU YA PAMBAZUKO

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Mhariri Mkuu** | : | Simon **MKINA** | (simon@pambazuko.or.tz) |
| **Mhariri Mtendaji** | : | Peter **NYANJE** | 0784 211 716 |
| **Mhariri wa Habari** | : | Maregesi **PAUL** | 0689 732 325 |
| **Mwandishi Mkuu** | : | Elizabeth **HOMBO** | 0712 792 216 |
| **Mwandishi Mwandamizi** | : | Andrew **MSECHU** | 0769 415 815 |
| **Mkuu wa DTP** | : | Yassin **LUPATU** | 0782 009 971 |
| **Mkuu wa Utawala** | : | Tryruckia **MFINANGA** | 0744 768 263 |

*Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz*

# Dunia: Hapa na pale

## Trump aweka kiburi zaidi

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amepuuza mwito wa kuomba radhi kwa familia ya aliyekuwa kiongozi wa nchi hiyo, Barack Obama na mkewe, Michelle, baada ya kusambaza kwenye mtandao wake wa kijamii Truth, picha iliyowadhihaki.

Katika picha hiyo, Obama na mkewe, walionekana kuwa na sura za sokwe.

Picha hiyo imezua hasira kubwa miongoni mwa viongozi wa kisiasa, wanaharakati wa haki za binadamu na umma kwa jumla, wakieleza kuwa ni ya kibaguzi na ya kudhalilisha.


Licha ya shinikizo la umma, Trump hajatoa kauli ya kuomba radhi, huku ikielezwa na watetezi wa Trump kwamba ana haki ya kujieleza na kutumia uhuru wake kwa mujibu wa katiba.

Wakosoaji wanasema kitendo hicho kinachochea chuki na kudhoofisha heshima ya kisiasa, huku wakimtaka Trump kuwajibika na kuondoa maudhui hayo.

## Papa amlilia Pengo

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki Duniani, Pope Leo XIV, ametoa salamu za rambirambi kufuatia kifo cha Kardinali mstaafu wa Tanzania, Polycarp Pengo, akimtaja kuwa mtumishi mwaminifu na mwenye kujitoa kwa Kanisa na taifa.

Katika ujumbe wake, Papa Leo alisema Kardinali Pengo alitumikia kwa unyenyekevu, hekima na ujasiri, akiongoza waumini katika nyakati mbalimbali za changamoto.



Alisisitiza kuwa mchango wake katika kuimarisha imani, maadili na mshikamano wa kijamii utaendelea kukumbukwa.

Waumini na viongozi mbalimbali duniani wameeleza masikitiko yao, wakimtaja marehemu kuwa kiongozi aliyelinda misingi ya imani na maadili ya Kikristo kwa moyo wa dhati.



## Traore akomesha rushwa

KIONGOZI wa Burkina Faso, Ibrahim Traoré, amesema serikali yake imefanikiwa kukomesha vitendo vya rushwa vilivyokuwa vimekithiri katika taasisi za umma, akisisitiza kuwa hatua hiyo imeimarisha uaminifu wa wananchi kwa serikali.

Traoré amesema mageuzi ya kiutawala, ukaguzi mkali wa matumizi ya fedha za umma na hatua kali dhidi ya watumishi wasiowajibika, vimeleta mabadiliko makubwa.

Aliongeza kuwa uwazi katika miradi ya maendeleo umeongezeka na mapato ya serikali sasa yanatumika kwa manufaa ya wananchi.

Rais huyo alieleza kuwa mapambano dhidi ya rushwa yataendelea kuwa kipaumbele ili kujenga taifa lenye nidhamu, uwajibikaji na maendeleo endelevu kwa watu wote.

## ODM wavurugana zaidi

CHAMA cha upinzani cha Kenya, Orange Democratic Movement (ODM), kilichoanzishwa na Raila Odinga, kimeingia katika mgogoro mkubwa wa kiuongozi huku baadhi ya “wakubwa waandamizi” wakishutumiana hadharani.

Chanzo cha mvutano huo ni madai ya ushirikiano wa karibu kati ya ODM na Serikali ya Rais William Ruto.

Baadhi ya wanachama wanapinga vikali wazo la chama hicho kuwa sehemu ya serikali au kushirikiana nayo kuelekea uchaguzi mkuu wa 2027, wakisema hatua hiyo itadhoofisha misingi ya upinzani.

Hata hivyo, wengine wanatetea mazungumzo ya kisiasa kama njia ya kuleta utulivu na maridhiano ya kitaifa.

Na Mzee TAI

Jicho la Tai

# Makonda kaiacha Arusha kuwa uji wa magimbi


Mbunge wa Arusha Mjini, Paul Makonda

HAKIKA uzee una mambo mengi sana. Yaani unaweza kupelekwa huku na kule – ukikwea ndege kwenda mji mmoja hadi mwingine na nchi hii ama ile. Huko haufikishwi kwa ajili ya utalii! La hasha, bali kuisaka tiba.

Sasa vijana wangu wamejikusanya baada ya kuona “kipresha” hakishuki. Wakaamua kunipeleka Arusha ambako mmoja wa vijana wangu anaishi. Kwamba huko kuna hospitali nzuri ya ugonjwa huo na mengine ya uzee.

Hata hivyo, baada ya kuwepo hapo kwa siku tatu, nikahisi kuwa jiji hilo la Arusha kama limepoa hivi. Halina tena pilikapilika kama zilizoanza kuzoeleka wakati wa Paul Makonda alipokuwa mkuu wa mkoa.

Wakati wa Gavana Makonda, mtu angeweza kabisa kuamini kuwa yapo baadhi ya maeneo yana roho. Na hakika – kwa muda fulani, roho ya Arusha ilikuwa ikidunda kwa kasi isiyo ya kawaida. Tangu aondoke Makonda, ambaye sasa ni mbunge na kubahatika kuwa waziri, mambo yamebadilika. Siyo kwamba Arusha imelala kabisa, Hapana, lakini imepoa. Imetulia, utadhani uji wa magimbi uliowekwa dirishani upoe haraka. Jiji limekuwa zito namna hiyo.

Wakati wa enzi za Makonda, Arusha haikuwa tu jiji la utalii; ilikuwa jukwaa la matukio. Leo kuchoma nyama pembezoni mwa barabara, kesho mashindano ya magari, mara mikutano ya ghafla, mara ziara za kushtukiza. Kila kona kulikuwa na jambo. Watu walikuwa hawaulizani - “kuna nini leo?” Bali - “leo kuna nini tena?”

Wachuuzi wa mishikaki walikuwa na wakati wao wa dhahabu. Mafundi wa spika na majukwaa hawakulala. Hata wapiga debe wa matukio walionekana kuwa na ajira ya kudumu.

Arusha ilikuwa kama tamasha lisiloisha. Wengine waliipenda hekaheka hiyo; wengine walishika vichwa – wakiamini ni vituko, kumbe ndiyo Makonda yuko kazini.

Sasa utulivu umetanda. Barabara hazina misafara ya ghafla. Hakuna tena mashindano yanayozua foleni za kusisimua. Wachoma nyama bado wapo, lakini hawachomi kwa presha ya ziara ya kushtukiza. Mitaa imebaki na upepo wake wa kawaida wa Mlima Meru.

Wapo wanaosema huu ndio “utawala wa kawaida.” Wengine wanamiss zile siku za pilikapilika.

Ukweli ni kwamba Makonda sasa ni mbunge na waziri; majukumu yake yamekuwa ya kitaifa zaidi. Hawezi tena kuikimbiza Arusha kila asubuhi na jioni kama zamani.

Mie mzee wenu sikasiriki kukosekana kwa Mkonda Arusha, bali naona ni fursa kwake kuanza kukimbiza sera, kusimamia bajeti na mijadala ya Bunge, kulea vyombo vya Habari na kujiepusha na ukandamizaji.

Hata hivyo, naona Arusha wanammiss na wenye jiji lao wanaona eneo lao limebaki kama kijana aliyemaliza shule ya bweni – tena inayoongozwa na masista wa Kikatoliki.

Kwa sasa, Arusha ipo kimya. Siyo kimya cha huzuni, bali kimya cha kupumzika. Na kama uji wa magimbi, huenda baada ya kupoa kidogo, ukawa mtamu zaidi.

Habari Kuu

# Ukata watafuna EAC




Na Mwandishi WETU

HALI mbaya ya kifedha imeikumba Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC) baada ya baadhi ya wanachama wake “kukacha” kulipa michango yao ya kila mwaka.

Shughuli kadhaa za EAC na taasisi zake nyeti; Bunge na Mahakama zimesitishwa kutokana na ukosefu wa fedha.

Kwa miaka kadhaa jumuia hiyo imekuwa ikitegemea fedha za wafadhili, lakini nazo sasa hazitoshi na kusababisha shughuli nyingi kusimama.

Bunge la Afrika Mashariki (EALA) halijafanya vikao kwa muda sasa kutokana na kukosekana kwa fedha za kuendesha vikao hivyo huku Mahakama ya Afrika Mashariki (EACJ) nayo ikilazimika kutosikiliza kesi kutokana na ukata.

Hali hiyo imemlazimisha mwenyekiti wa jumuia hiyo hivi sasa, Rais William Ruto wa Kenya, kuitisha kikao cha dharura cha wakuu wa nchi mwezi ujao jijini Arusha ili kuweka mkakati mpya wa kukusanya fedha kwa ajili ya uendeshaji wa jumuia hiyo yenye wanachama nane hivi sasa.

Kikao hicho cha wakuu wa nchi kimepangwa kufanyika Machi 7 jijini Arusha, kikiwa ni kikao cha kwanza cha viongozi hao katika kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja.

Kwa kawaida wakuu wa nchi wanapaswa kukutana angalau mara moja kwa mwaka, lakini hawajafanya hivyo kutokana na suala hilo la ukata.

Katika kikao hicho viongozi hao wanatarajia kujadili mikakati na utaratibu mpya na mzuri wa kukusanya fedha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za jumuia.

Pia wanatarajiwa kujadili mikakati ya kubana matumizi na kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana kwa matumizi yatakayofanyika hasa kwenye miradi.

Rais Ruto amesisitiza viongozi wote wakuu wa nchi kuhudhuria kikao hicho wao wenyewe akikitaja kuwa ni muhimu sana kwa mustakabali wa jumuia hiyo ambayo inapigiwa mfano katika Afrika.

Hadi hivi sasa, kwa ujumla, wanachama wa jumuia hiyo wanadaiwa zaidi ya dola za Marekani milioni 89.3 (zaidi ya shilingi bilioni 230) kutokana na kushindwa kutoa michango yao ya ada za mwaka kwa wakati.

Jumuia imekuwa na ukata kiasi kuwa hata shughuli za sekretarieti zimekwama na hivyo kuleta wasiwasi mkubwa kuhusiana na mustakabali wa jumuiya hiyo.

Haitashangaza iwapo viongozi hao watakuja na mfumo mpya wa kukusanya fedha kwa ajili ya shughuli za jumuia.

Inaendelea Uk.7

# Ukata watafuna EAC

Inatoka Uk. 6

Waziri wa Masuala ya Afrika Mashariki wa Kenya, Beatrice Askul, amethibitisha kuwa suala la ukata wa jumuia ndio ajenda muhimu katika kikao hicho.

Akizungumza na vyombo vya habari hivi karibuni, alisisitiza kuwa wakuu wa nchi ndio wenye mamlaka ya mwisho kuhusu masuala ya kisera na kifedha yanayoihusu jumuia.

Wachambuzi wa mambo wanaamini kuwa kikao hicho ni muhimu sana kwa mustakabali wa jumuia hiyo.

### Madeni yarundikana

Kwa muda mrefu nchi wanachama wamekuwa wakisuasua kulipa michango yao na hivyo kukwamisha shughuli za jumuia.

Januari 31, 2026, EAC ilikuwa inazidai nchi wanachama jumla ya dola za Marekani milioni 89.372 za michango ambayo ilikuwa haijalipwa.

Katika taratibu za sasa, kila nchi mwanachama inapaswa kuchanga dola milioni saba kwa mwaka ikiwa ni ada ya uanachama.

Kwa kiasi kikubwa fedha hizo ndizo zinatumika kugharamia shughuli za sekretarieti, bunge na mahakama, huku kiasi fulani kikielekezwa kwenye miradi.

Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ni Kenya na Tanzania pekee ndizo zimekamilisha malipo ya ada zao za uanachama.

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ndiyo ina deni kubwa la dola milioni 27, ikifuatiwa na Burundi inayodaiwa dola milioni 22.7 huku Sudani Kusini ikidaiwa dola milioni 21.8.

Somalia ina deni la dola milioni 10.5 na Rwanda inadaiwa dola milioni 5.2 huku deni la Uganda likiwa ni dola milioni 1.1.

Utaratibu huu wa nchi kukacha kulipa ada zao umekuwepo kwa kipindi kirefu hadi hivi sasa hali imekuwa mbaya sana.

Kwa muda mrefu uendeshaji wa jumuia ulikuwa ukitegemea fedha za wafadhili ambazo nazo zina kikomo chake.

### Shughuli zakwama

Ukata huo mkubwa umesababisha madhara makubwa kwa shughuli za jumuia. Kutokana na upungufu wa fedha baadhi ya mambo yanayopaswa kufanywa na EAC sasa yamekuwa yakifanyika kwa kiwango kidogo huku mengine yakikwama kabisa.

Ukiacha kukwama kwa shughuli za sekretariati, taasisi nyingine ikiwamo EALA nazo zimeathirika.

EALA, ambayo jukumu lake kubwa ni kupitisha sheria, imelazimika kuahirisha vikao vyake kwa muda mrefu kutokana na kukosa fedha.

Taarifa zinaonyesha kuwa Wabunge wa EALA hawajalipwa stahiki zao tangu Novemba mwaka jana na kufanya shughuli za bunge hilo kusitishwa.

Kwa upande mwingine, EACJ, chombo ambacho kinapaswa kusimamia utekelezaji wa sheria na mkataba wa EAC, nayo imeathirika.

Hali hiyo inatishia imani ya wadau wa EAC hasa wawekezaji na wafanyabiashara kwani sasa hakuna jambo kubwa linalofanywa na jumuia hiyo. Mahakama hiyo pia husikiliza kesi za migogoro ya kibiashara na uwekezaji na kukwama kwake kufanya kazi kunatishia maslahi ya wafanyabiashara na wawekezaji kutoka ndani na nje ya Afrika Mashariki. Utekelezaji wa miradi na programu nyingi zinazoendeshwa na EAC nao umekwama kutokana na kukosekana kwa fedha.

Wakala kadhaa za jumuia hiyo nazo zimekwama kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mathalani, taarifa zinaeleza kuwa Inter-University Council of East Africa inadai kiasi cha dola milioni 18.4, Lake Victoria Fisheries Organisation inadai dola milioni 2.1 huku Civil Aviation Safety and Security Oversight ambayo ina makao yake Kampala Uganda ikidai dola milioni 3.1.

Awali, suala hili lilianza kama ucheleweshaji wa fedha kwa ajili ya programu na miradi lakini sasa limegeuka kuwa mgogoro wa kiuchumi unaokwamisha utekelezaji wa miradi na programu.

### EAC imefikaje hapo?

Ukata huu mkubwa unaoshuhudiwa unatokana na mambo mawili makubwa. Kwanza ni muundo wa jumuia yenyewe na pili ni hali ya kisiasa kwa baadhi ya nchi wanachama.

Inaendelea Uk.8

# Ukata watafuna EAC

Inatoka Uk. 7

Kwa miaka kadhaa sasa wachambuzi wamekuwa wakikosoa utaratibu wa wanachama kuchangia shughuli za Jumuiya kwa usawa.

Wachumi wanabainisha kuwa utaratibu wa sasa wa kutoa kiwango sawa cha ada ya uanachama si wa haki kwa sababu uchumi wa nchi hizo wanachama haulingani.

Ukiacha Kenya, Tanzania na Rwanda ambazo uchumi wake unaonekana kuwa nafuu, EAC inaundwa pia na nchi ambazo uchumi wake uko taabani kama ilivyo kwa Somalia, Sudani Kusini na Burundi.

Kwa upande mwingine, nchi za DRC, Sudani Kusini, Somalia na hata Burundi kwa miaka mingi zimekuwa zikisumbuliwa na migogoro ya kisiasa isiyokwisha.

Hali ni mbaya zaidi DRC ambayo kwa miaka mingi imekuwa ikikabiliana bila mafanikio na makundi ya waasi hasa katika eneo la mashariki.

Somalia nayo haijatulia kwani kwa miaka mingi imekuwa katyika mapambano na makundi ya waasi na magaidi.

Katika hali kama hiyo, wachambuzi wanasdema kuwa ni vigumu sana kwa kila nchi kutoa mchango sawa na nchi nyingine.

Kwa upande mwingine, kila nchi kati ya wanachama inakabiliwa na tatizo sugu la madeni ya nje, kuyumba kwa thamani ya sarafu zao na ufinyu wa makusanyo ya mapato.

Katika mapambano hayo ya uchumi, ni dhahiri kuwa michango ya EAC haiwezi kuwa kipaumbele cha nchi hizo.

Kupanuka kwa Jumuiya hiyo kwa kasi katika miaka ya hivi karibuni nayo imetajwa kama sababu ya ukata uliopo hivi sasa.

Tangu 2016, EAC imepokea wanachama kadhaa wapya ikiwamo Sudani Kusini, DRC na Somalia.

Hii imesababisha rasilimali chache zilizopo kulazimika kufanya majukumu mengi bila ya kuwepo kwa mabadiliko ya uchagiaji.

Mwisho, kuwepo kwa mifumo dhaifu ya kuhakikisha utekelezaji wa majukumu baina ya nchi wanachama.

Mathalani, hakuna adhabu ya maana ambayo nchi isiyolipa michango inayopata na kuzifanya nchi hizi kubweteka kulipa michango yao.

### Kuwatisha wawekezaaji

Hali hii tete kifedha inakuja wakati Afrika Mashariki ikijipigia upatu kama eneo linalofaa zaidi kuwekeza katika Afrika kwani lina mambo yote ya msingi ambayo wawekezaji yanawafaa likiwemo soko lenye watu milioni 300.

Pia, Afrika Mashariki inajitaja kama daraja kati ya maeneo ya kuichumi kama vile Mpango wa Eneo la Biashara Huru wa Afrika (AfCFTA), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Soko la Pamoja la Mashariki na Kusini mwa Afrika (Comesa).

Lakini sifa zote hizi zimetiwa dosari na hali hii ya ukata, jambo ambalo linaweza kuwatisha wawekezaji.

### Nini kifanyike?

Wachambyzi wa masuala ya uchumi wanashauri kuwa ni wakati sasa wanachama wa EAC wakaja na mfumo mpya wa kuchangia shughuli za jumuia.

Wanashauri kuwa michango inafaa itokane na hali ya uchumi wa nchi kwa kupima pato la taifa yaani GDP.

Wanasema hali hii italeta usawa wa uchangiaji kwani nchi zenye uchumi dhaifu zitachangia kidogo kulingana na uchumi wao huo zile zenye uchumi miubwa zikichanga zaidi kwano nazo zinanufaika zaidi kutokana na uwezo wake mkubwa wa kufanya biashara ndani ya jumuia.

Wachambuzi wanashauri pia uanzishwe utaratibu wa kuziadhibu nchi ambazo zinachelewesha michango yao.

Wanasewma utaratibu huo utaleta nidhamu ya uchangiaji.

Pia kuna haja ya jumuia kupanua vyanzo vya mapato kwa kuweka ushuru wa aina fulani katika baadhi ya bidhaa hasa katika biahara baina ya nchi.

Kwa upande mwingine wanashauri pia Jumuiya ichunge matumizi yake na kuepuka matumizi yasiyo la lazima.

Mwisho wanashauri kuwepo kwa uwajibikaji wa kisiasa ambao utailazimisha kila nchi kuweka kipaumbele kwa shughuli za jumuia.



# Bandari 'kuchangamsha' Katavi kiuchumi

*Moja ya meli zinazoendelea kujengwa kwenye Bandari ya Karema. (Na Mpigapicha Maalum*

**Na Mwandishi WETU**

MKOA wa Katavi sasa 'utachangamka' zaidi baada ya kukamilika na kuanza kazi kwa meli nne zinazoendelea kujengwa Bandari ya Karema.

Bandari hiyo iliyoko Wilaya ya Tanganyika ni chachu yenye kuchochea maendeleo ya wananchi, huku serikali ikipata manufaa makubwa yanayotokana na kodi.

Katika kuhakikisha maendeleo hayo ya kazi yanayosukumwa na uwepo wa meli, serikali imekuwa ikifuatilia kwa ukaribu kukamilika kwa ujenzi wake.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile alitembelea eneo la ujenzi wa meli hiyo katika Badari ya Karema na kuona namna mafundi wanavyofanya kazi zao.

Naibu Waziri huyo alifurahishwa na kasi ya ujenzi wa meli hizo huku akipongeza hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa meli hizo nne unaoendelea.

Kihenzile alisema serikali imeweka mikakati mahsusi ya kuhakikisha maeneo yenye bandari yanakuwa chanzo kikubwa cha mapato na manufaa kwa wananchi na nchi kwa ujumla wake.

Mradi wa ujenzi wa meli hizo nne unafanywa kwa ubia kati ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) na kampuni ya Gold Voyage Logistics kutoka nchini China.

"Meli hizi zitakwenda kuongeza tija kwenye bandari zetu kwa sababu zitakuwa zinabeba mzigo kutoka nchi jirani za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Burundi na Zambia kuleta upande wetu kupitia bandari za Ziwa Tanganyika kabla ya kupokelewa Bandari ya Dar es Salaam na kusafirishwa popote duniani," alisema Kihenzile.

Aidha, Kihenzile alitoa mwaliko kwa sekta binafsi kuwekeza zaidi katika sekta ya uchukuzi ili kuongeza ufanisi katika usafiri na usafirishaji.

Awali akiwasilisha taarifa ya uendeshaji wa Bandari ya Karema, Meneja wa Bandari za Ziwa Tanganyika, Edward Mabula alisema kuwa ujenzi wa meli tatu umekamilika na meli moja imefikia asilimia 90 na inatarajiwa kukamilika muda si mrefu.

Mabula alisema kuwa tangu bandari hiyo kuanza imehudumia tani 15,000 za mizigo, meli saba na boti takribani 600 jambo linaloonesha kuwa bandari hiyo bado haijatumika ipasavyo, lakini akasema kuwa miundombinu itakapokamilika, ikiwamo ya ujenzi wa meli hizo nne utakapokamilika na kuanza kazi, itakuwa na ufanisi unaotakiwa na hata kupita matarajio.

Tafakuri ya Bagonza



Na Dkt. Benson BAGONZA

# Tuomboleze kwa pamoja na TEC



*Muadhama Kardinali Pengo*

KANISA Katoliki limempoteza mmoja wa viongozi wake.

Ni Muadhama Polycap Kardinali Pengo. Baraza la Maaskofu (TEC) limempoteza jabali wa Maadili ya Kanisa.

Taifa limempoteza kiongozi wa kijamii aliyekuwa tayari wakati wote kutoa mawazo yake kwa ajili ya ustawi wa jamii nzima.

Msiba huu umetukuta katikati ya msiba mwingine. Viongozi wetu wametawanyika huko huko kuzima mioto mbalimbali. Kwa hiyo, tunapoomboleza msiba wa Muadhama Pengo, ni muhimu "kuomboleza vizuri."

Napenda kushauri yafuatayo;

Ieleweke kuwa Muadhama Pengo na Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) havitenganishwi.

Huwezi kumpenda Pengo ukaichukia TEC au kinyume chake. Tumia hekima kama huna akili ya kutumia.

Ni kweli kwamba Kanisa Katoliki limeumizwa na wasioujua muundo wake. Kwenye msiba huu ni vyema sana "vijora viwe likizo." Kama kuna ulazima wa kutumika basi, vitumike wakati mwingine. Asiyependa kuomboleza, awape nafasi wanaoomboleza.

Muadhama Pengo ni bingwa wa Maadili ya Kiroho. Kama hukuwa naye siku za mwisho, usikimbilie kubuni alikuwa anawaza nini. Hali yake na msimamo wake wa mwisho anaujua yeye na Muumba wake. Letu ni kumuombea, si kummiliki.

Muadhama amefanya kazi na marais wote sita. Anawajua wote. Wanamjua kwa sehemu tu. Hilo ndilo kanisa. Marais wema na wabaya huja na kupita. Kanisa hubaki. Tusilibeze kanisa linalobaki wakati sisi tunapita. Machawa nimewawashia taa msije sema sikuwaambia.

Muadhama Pengo alikuwa Mkristo, Mkatoliki. Hakuna ukatoliki usio ukristo hata kama kuna ukristo usio ukatoliki. Kiunganishi ni msalaba. Jitihada za kuliunganisha Taifa, ZISIJARIBU kuwagawa wakristo kati ya TEC, CCT, PCT, SDA nk. Wote ni Wakristo hata kama kuna wanaoweza kuwepo wanaojiona bora kuliko wengine. Kanisani hakuna cha "Kanisa lina wenyewe".

Muadhama Pengo alikataa katakata dhana ya dini ya Taifa. Haikufaa na haitafaa. Wakristo wanaojifanya ni wakristo kuliko Bwana Yesu, Paeni mbinguni mkaishi huko.

Wale ndugu zangu wanaojifanya wana dini kuliko Mtume, nendeni muishi huko alikozaliwa. Tanzania yetu sote, wanaovaa vimini na baibui. Muadhama alipenda ukweli kama unavyosimamiwa na TEC. Tushawishiane, tusiburuzane.

Pumzika Mzee wetu. Hata Wajaluo wanakulilia.

Kwaresima Njema: Ramadhani Kareem.

***Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.***


Na Dkt. Hellen Kijo BISIMBA



Kona ya Dkt. Bisimba

# Mbuyu wa haki wang'oka kwa heshima

SIDHANI kama nina maneno ya kutosha kuandika buriani kwa mwanaharakati mahiri wa haki za kiraia, kijamii na utu wa watu, Mchungaji Jesse Jackson wa Marekani, aliyefariki dunia kwa heshima akiwa nyumbani kwake Februari 17, 2026.



Wengi wametoa heshima zao wakimuelezea alivyokuwa mtu wa haki na kiongozi muadilifu kiasi cha kumtaja kuwa ni 'Jitu la Maadili' (Moral Giant).

Mchungaji Jackson (pichani) ni Mmarekani mweusi aliyezaliwa Oktoba 8, 1941 huko Carlifonia, Marekani.

Nimeguswa sana na jinsi Mchungaji huyu wa Kanisa la Kibaptisti alivyoshindwa kuvumilia ubaguzi wa rangi na sheria za kibaguzi kiasi cha kujiunga katika harakati za kupinga ubaguzi.

Niliona jinsi alivyokuwa jasiri hadi kutokea kuwa kiongozi wa jopo la haki za kiraia baada ya kifo cha mtangulizi wake, mwanaharakati wa haki za raia Mchungaji Dkt. Martin Luther King Jr.

Nililojifunza kwake ni ushupavu, kwani siku Dkt. King anauawa, yeye alikuwa miongoni mwa watu waliokuwa wanamsikiliza.

Dkt. King aliuawa akiwa katika harakati za kutafuta haki ya usawa. Kifo cha Dkt. King hakikumrudisha nyuma, bali kilionekana kuwa kichocheo cha yeye kukamata usukani ili haki za watu ziheshimiwe na sheria zote za kibaguzi ziondolewe.

Aliweza kuanzisha mtandao uliojulikana kwa jina la Rainbow PUSH akiwaunganisha watu kupambania haki za kiraia na kijamii.

Nikimtafakari Mchungaji Jesse Jackson na mtangulizi wake, Dkt. King, ninajiuliza ni kwa nini wapo watu wa aina zao (viongozi wa kidini) wanaoshindwa kusimama pale wanapoona dhahiri haki zinadhulumiwa na kukiukwa?

Pia ninashangazwa na wanaharakati ambao wameanza kazi ya kupambana dhidi ya uonevu, lakini wakiona watu wamekamatwa, wameteswa au kupotezwa, kuuawa, wanarudi nyuma na kuacha kabisa utetezi.

Mchungaji Jesse amekuwa kioo, nembo na alama ya haki za usawa wa rangi na za binadamu akipinga ubaguzi wa rangi popote ulipo, hata Afrika Kusini.

Nimeona jinsi Shirika la Nelson Mandela la Afrika Kusini lilivyomlilia likisema alikuwa mwanaharakati aliyepinga uonevu na ubaguzi, ambaye aliwahi kushinikiza Mandela aachiwe huru na hata alipoachiwa alifika Afrika Kusini kusherehekea kuachiwa kwake.

Kifo cha Mchungaji Jackson kumeinua hali ya ukuu wa urathi wake, kwani dunia nzima zimesikika sifa zake hata marais watatu nchini Marekani wote wametoa rambirambi na sifa kuu za mwanaharakati huyu mahiri anayetajwa kuwa kiongozi mfuasi, mwenye nguvu ya kuleta mabadiliko.

Baada ya kifo cha Martin Luther aliyeuawa akiwa na umri wa miaka 30 tu, Mchungaji Jackson aliendelea kuandaa maandamano na majadiliano akipaza sauti dhidi ya ubaguzi.

Kifo hakikumtisha hadi amehitimu maisha akiwa na miaka 84.

Atakumbukwa zaidi kwa jinsi alivyoukimbiza mwenge wa haki za kiraia kwa ushupavu mkuu hata kugombea urais wa Marekani mara mbili ili kukuza ndoto ya mabadiliko nchini kwao.

Urathi wake mkuu pia ni kwa kiasi alivyokuwa mtu mkweli bila kuogopa wenye mamlaka na bila kujali ukimya wa wengi. Amekuwa akivikumbusha vizazi kuhakikisha tumaini linaendelea kuishi.

Tunashukuru Mungu kwa maisha ya Mchungaji Jackson, tunatoa pole kwa familia, wanaharakati wote wa haki duniani, bado lipo tumaini.

***Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.***

Makala

# Dkt Nchemba achefukwa madudu serikalini



*Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu Nchemba*

Na Mwandishi WETU

NCHI hii inapigwa na wapigaji hawana huruma. Unaweza usiamini na wakati mwingine usielewe ni kwanini baadhi ya watumishi wa umma ni wazembe, hawatimizi wajibu wao inavyotakiwa na "wanatafuna" fedha za umma bila huruma.

Watumishi hao wana uhakika wa kulipwa mishahara kila mwezi, wanalipwa stahiki zao kulingana na mikataba ya ajira zao na pia wanalipwa marupurupu na fedha zingine wanazostahili kulipwa, lakini ni wala rushwa.

Wapo watumishi wanaochelewa kufika ofisini bila sababu za msingi, wapo watumishi wenye mamlaka, lakini hawataki kuwatendea haki watumishi wenzao na wananchi kwa mujibu wa sheria za utumishi wa umma na watumishi wengine wanakwamisha miradi ya maendeleo kwa masilahi yao binafsi.

Kutokana na mazingira hayo, baadhi ya watumishi wazembe na wasiotimiza wajibu wao, wamekuwa wakiichonganisha serikali na wananchi na mara kadhaa wananchi wanaiona serikali haiwatendei haki kwa sababu hawapati haki wanazostahili kupata.

Yaani, kuna mahali wananchi hawapati dawa hospitalini, wanafunzi wanasomea chini ya miti kwa sababu ya ukosefu wa majengo, wanafunzi wanajisaidia porini kutokana na ukosefu wa vyoo na baadhi ya watumishi wanakwamisha miradi mbalimbali ikiwamo miradi ya maji, barabara, umeme na mingine kwa sababu zao binafsi.

Madudu hayo yameendelea kujidhihirisha wiki iliyopita, wakati Waziri Mkuu, Dkt. Mwigulu Nchemba, alipofanya ziara ya kiserikali mkoani Tanga.

Akiwa katika ziara hiyo, waziri mkuu hakuamini macho yake, kwani alishuhudia jinsi fedha za umma zinavyotafunwa na wachache na zingine zinavyopotea kutokana na uzembe wa watumishi wa umma.

Pia, waziri mkuu alishuhudia jinsi miradi ya maendeleo inavyokwama kutokana na uzembe wa baadhi ya watendaji wa serikali na pia alipokea malalamiko yanayoonyesha jinsi watumishi wa umma wasivyoweza kutatua kero za wananchi.

Wakati wa ziara yake mkoani humo, mara kadhaa waziri mkuu alikuwa akifoka na kuwakemea watumishi wa umma wasiotimiza wajibu wao na wakati huo huo akitoa maelekezo kwa watumishi wote.

Ili kuokoa fedha za umma zinazotafunwa, wakati akihitimisha ziara hiyo, Waziri Mkuu alimwagiza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tamisemi, Profesa Riziki Shemdoe, arudi katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ili akawachukulie hatua watumishi wote waliohusika na ubadhirifu wa fedha za mradi wa jengo la ofisi za wilaya hiyo.

Inaendelea Uk. 13

# Dkt Nchemba...

Inatoka Uk. 12

Alitoa agizo hilo wakati akizungumza na viongozi na watumishi wa Mkoa wa Tanga, katika kikao cha majumuisho ya ziara yake ya siku tano mkoani humo yaliyofanyika kwenye Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto.

"Muheza ndiyo wilaya iliyonikera, mheshimiwa waziri kesho rudi Muheza, nenda kachukue hatua, shirikiana na waziri wa utumishi, mchukue hatua…"

"Kule kuna baadhi ya vifaa vya ujenzi vilinunuliwa, lakini havikufika site, nondo zenye thamani ya shilingi milioni 9.2 zililipwa kwa mzabuni Saifi Store wa Tanga, lakini hazikufikishwa site, maana yake zimechepushwa…"

"Kuna marine boards vipande 192 vyenye thamani ya shilingi milioni 7.8 havikufika site, wanaohusika ni mhasibu na mhandisi na ofisa anayehusika kupokea vifaa…"

"Mbali ya hayo, kuna malipo mengine ya shilingi milioni 4.4 yalifanywa ili kulipia mifuko 3,800 ya saruji, lakini mifuko 300 haikufika kwenye eneo la ujenzi. Ofisa manunuzi na ofisa utumishi ambaye alikuwa ni mwenyekiti wa kamati ya mapokezi ya vifaa vya mradi, watafutwe hawa pamoja na Mkurugenzi wa Mwanambonde General Enterprises," alisema waziri mkuu.

Waziri Mkuu alisema kuna ukiukwaji wa taratibu za serikali uliofanyika kinyume cha utaratibu ikiwamo kumlipa mshauri mwelekezi bila kuwa na mkataba wowote.

"Kuna huyu AG Engineering amelipwa shilingi milioni 98.7 bila kuwa na mkataba, alilipwa za nini na kuna mshauri mwelekezi alilipwa shilingi milioni 11.9 bila mkataba…"

"Kibaya zaidi, shilingi milioni 343 zimetumika nje ya mradi kwa kulipana posho. Mheshimiwa Waziri, nenda kasafishe wote pale. Safisha wote pale hii wilaya ianze upya. Ongea na Waziri wa Utumishi kila mmoja apate adhabu anayostahili," alisema.

Pamoja na ubadhirifu huo, awali Waziri Mkuu alipokuwa wilayani Handeni, alisema serikali ilipeleka wilayani humo mifuko 1262 ya simenti kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha VETA.




*Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu Nchemba akiwa katika ziara mkoani Tanga hivi karibuni. (Picha na Tovuti ya Waziri Mkuu)*

Badala ya mifuko hiyo kutumika katika ujenzi kama ilivyoelekezwa, waziri mkuu alisema mifuko hiyo iliganda na kuharibika, jambo ambalo alisema hawezi kulikubali.

Pamoja na uharibifu huo, Nchemba alishangaa watumishi waliosababisha uovu huo, kuendelea kufanya kazi serikalini huku wakiendelea kulipwa mishahara kila mwezi wakati hawatimizi wajibu wao.

Ili kuonyesha jinsi alivyokerwa na uzembe huo, alimwagiza Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, awachukulie hatua watumishi wote waliosababisha uharibifu wa mifuko hiyo na pia wakatwe mishahara ili mifuko mingine ya simenti inunuliwe kwa ajili ya ujenzi wa chuo hicho.

"Mkuu wa mkoa, Waziri wa Tamisemi na Waziri wa Elimu, watafuteni wote waliosababisha mifuko hiyo kuganda na wakatwe mishahara yao maana kama mifuko hiyo ingekuwa mali yao, isingeganda," aliagiza.

Katika hatua nyingine, alikemea tabia ya watumishi wa umma kufanya kazi kwa mazoea na kusema yeyote anayeona hawezi kufanya kazi serikalini, aache kazi ili nafasi yake ijazwe na wengine wenye moyo wa kufanya kazi kwa uadilifu.

Inaendelea Uk. 14

# Dkt Nchemba...

Inatoka Uk. 13

Wakati huo huo, Waziri Mkuu alishangazwa na utaratibu wa viongozi wa wilaya hiyo, kuagiza simenti jijini Dar es Salaam na Mbeya kwa ajili ya ujenzi wa majengo wilayani humo, wakati mkoani Tanga kuna viwanda vinne vya simenti.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, uagizwaji huo wa simenti ni njia mojawapo ya kufuja fedha za umma na kwamba utaratibu huo unatakiwa kukoma mara moja.

**Tanga Mjini**

Akiwa jijini Tanga, Waziri Mkuu alieleza jinsi uongozi wa jiji hilo ulivyoshindwa kujenga majengo ya vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo katika Shule ya Sekondari Chongoleani licha ya Serikali kupeleka fedha kwa ajili ya majengo hayo, Machi 4, mwaka jana.

Waziri mkuu alishikwa na mshangao kwa uwepo wa hali hiyo na kuwashangaa Mkurugenzi wa Jiji la Tanga pamoja na ofisa elimu wa mkoa huo, kuvaa vizuri na kupendeza wakati wanafunzi wanasomea katika mazingira mabovu.



*Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu Nchemba akimjulia hali Mbunge wa Moshi Mjini, Ibrahim Shayo aliyelazwa katika Hospitali ya KCMC Moshi, Kilimanjaro baada ya kupata ajali eneo la Kirinjiko, wilayani Same mkoani humo juzi. Kushoto ni Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Florence Samizi. (Picha na OWM).*

**Wilayani Lushoto**

Akiwa wilayani humo, pamoja na mambo mengi aliyokemea, Waziri Mkuu alieleza jinsi mkandarasi alivyotoroka baada ya kulipwa sh milioni 900 za Serikali kwa ajili ya kujenga mradi wa maji wilayani Korogwe.

Aliagiza mkandarasi huyo atafutwe mahali popote alipo, akamatwe na afikishwe katika vyombo vya dola ili arudishe fedha alizolipwa.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu, aliviagiza vyombo vya ulinzi na usalama mkoani Tanga, kumkamata na kumchukulia hatua za kisheria mwanaume wa miaka 53 anayetuhumiwa kumpa ujauzito binti mwenye umri wa chini ya miaka 18, katika Kata ya Mlalo, Wilaya ya Lushoto. Wakati akizungumzia suala hilo kwenye uzinduzi wa mitambo ya kuzalisha hewa ya oksijeni katika Hospitali ya Wilaya ya Lushoto, Waziri Mkuu alionyesha kuwapo kwa mazingira ya rushwa katika kushughurikia suala hilo kwa kuwa mtuhumiwa huyo yuko uraiani ingawa alitenda kosa.

"Kwa hiyo, Takukuru fuatilieni suala hilo kwa kina ili kubaini hatua zilizochukuliwa hapo awali na sababu mtuhumiwa kubaki huru bila kufikishwa mahakamani ni jambo linalotia shaka…:

"Iwapo mtumishi wa umma atabainika kuhusika kukwamisha haki au kumsaidia mtuhumiwa kwa njia yoyote ikiwemo rushwa, hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yake,"alisema.

**Wilayani Muheza**

Alipokuwa akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Lusanga, Kata ya Mgomeni, wilayani humo wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi la ofisi ya halmashauri hiyo, Waziri Mkuu alionyesha kukerwa na upotevu wa vifaa vya ujenzi wa jengo la serikali.

"Kuna nondo 700, marine boards 500 na matofali 2,000, hivi vifaa havijulikani viko wapi. Wahusika kila siku mnaripoti kazini na mishahara mnalipwa wakati ujenzi umesimama na hakuna hatua zinazochukuliwa.

"Kamanda wa Takukuru ninahitaji hii taarifa kwa kina kabla sijamaliza ziara yangu mkoani Tanga," aliagiza waziri mkuu.

# Giza nene utekelezaji Sheria Ununuzi wa Umma

Na Elizabeth HOMBO

MAMLAKA za Ununuzi wa Umma Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam, zimetakiwa "kuamka" na kuanza kutekeleza majukumu yake ipasavyo ili wananchi wanufaike na mifumo ya ununuzi nchini.

Wajasiriamali kadhaa kutoka manispaa hiyo waliozungumza na Pambazuko wamesema wengi wao hawana ufahamu na uelewa kuhusu mifumo ya ununuzi kwa sababu mamlaka zenye wajibu wa kuwapatia elimu hiyo hawajatekeleza wajibu wao ipasavyo.

Pambazuko liliwahoji wajasiriamali hao kutaka kujua kwa nini hawachangamkii fursa zinazotolewa kwa makundi maalum katika mfumo wa ununuzi nchini.

Wengi wao walionyesha kutokuwa na taarifa kuhusiana na mifumo hiyo wala upendeleo ambao umewekwa kisheria kwa ajili ya kuwanufaisha wajasiriamali kutoka makundi ya wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu.

Wajasiriamali wengi walisema hawana taarifa kuwa asilimia 30 ya zabuni katika ununuzi zinatengwa kwa ajili ya makundi hayo. Jambo ambalo limewafanya wengi wabweteke bila kuzitumia fursa hizo.

Walisema katika kipindi hiki ambacho kila mmoja anahangaika kutafuta namna atakavyotengeneza fedha kama wangefahamu fursa hiyo ingewasaidia sana wao kujiimarisha katika shuguli zao za ujasiriamali.

Licha ya kutenga asilimia 30 ya miradi ya ununuzi kwa ajili ya makundi hayo, sheria pia inaziwajibisha mamlaka za ununuzi kutoa elimu kwa umma, hususani kwa makundi hayo, kuhusiana na fursa hizo, ili waweze kuzitumia ipasavyo.

Uchunguzi wa Pambazuko umebaini kuwa elimu hiyo haitolewi ipasavyo huku watendaji katika ngazi mbalimbali wakilalamikia ufinyu wa bajeti kuwa ndio kikwazo cha wao kushindwa kutekeleza wajibu wao huo.



### Sheria inavyotaka

Kifungu cha 73(1) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya 2023, kinazitaka taasisi zote za umma kuhakikisha kuwa kazi za ununuzi, ugavi na uondoshaji mali zinafanywa na kutolewa taarifa kupitia mfumo wa kielektroniki wa manunuzi ya umma (NeST).

Sheria pia inaagiza kuwa asilimia 30 ya zabuni zote zinazotolewa zitengwe kwa ajili ya makundi maalum yanayojumuisha wanawake (asilimia 5), vijana (asilimia 10), wazee (asilimia 5) na watu wenye ulemavu (asilimia 10).

Kanuni ya 34(2) ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) ya mwaka 2024, inatamka kuwa chombo kinachohusika na makundi maalum lazima kihakikishe kuwa mafunzo muhimu yanatolewa kwa vikundi hivyo kabla ya kupewa cheti cha usajili ili viweze kushiriki kwenye mchakato wa ununuzi wa umma.

Sheria hiyo ilitoa upendeleo kwa makundi hayo kupata fursa ya kupata zabuni ili kusaidia kukuza biashara ndogo ndogo kama njia ya kupunguza ukosefu wa ajira.

### Mwongozo wa PPRA

Ili kuhakikisha kuwa makundi hayo yanashiriki kwenye mchakato wa ununuzi wa umma, PPRA imeandaa mwongozo maalum kwa ajili ya makundi hayo.

Mwongozo huo unaelekeza kuwa katika hizo asilimia 30, vijana wanapaswa kupata asilimia 10 ya zabuni zilizotengwa, watu wenye ulemavu asilimia 10, wanawake na wazee asilimia 5 kila kundi.

Inaendelea Uk. 16

Habari

# Giza nene utekelezaji Sheria Ununuzi...

Inatoka Uk. 15

**Giza nene Ubungo**

Licha ya upendeleo uliowekwa kisheria, Pambazuko limebaini kuwa bado makundi hayo hayanufaiki katika Manispaa ya Ubungo na watendaji wa manispaa hiyo wamekiri hilo.

Akizungumza na Pambazuko ofisini kwake juzi, Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi wa Manispaa ya Ubungo, Mvano Kalumbete, anasema malengo ya utekelezaji wa asilimia 30 kwa makundi maalum haujafikiwa kama ambavyo unatakiwa.

Anasema ni ngumu sana kwa jambo hilo kufanikiwa kutokana na changamoto kadhaa.

Miongoni mwa changamoto alizozitaja ni pamoja na bajeti ambayo inategemeana na makusanyo ya halmashauri kwa mwaka husika.

"Unajua halmashauri ina-run (inajiendesha) kwa bajeti iliyoko kwenye maandishi sio kwenye cash bajeti. Kwa hiyo, mfano unaweza kusema mwaka huu tutakuwa na zabuni labda za shilingi milioni 40, lakini mpaka mwaka unaisha mnajikuta mmepata shilingi milioni 20 tu.




*Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu, akiwa amebeba mikoba yenye nyaraka mbalimbali za kisheria kwa ajili ya kujitetea kwa kesi ya uhaini inayomkabili katika Mahakama Kuu ya Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. (Na Mpigapicha Wetu)*

"Inakuwa haijafikia ile lengo la shilingi milioni 40 kwa hiyo matokeo yake hautatekeleza manunuzi uliyokusudia kwa mwaka husika," anasema Kalumbete.

Aliitaja changamoto nyingine kubwa kuwa ni suala la mifumo ya NeST ambayo imegawanyika katika makundi mawili.

Anasema kuna NeST ndogo (NeST Mobile App) ambayo hutumika na halmashauri nyingi katika ununuzi wa kazi za ngazi za chini kama vile vifaa na ujenzi wa shule, vituo vya afya na zahanati. Kundi la pili ni NeST kubwa ambayo inafanya kazi makao makuu.

"Sasa huku kwenye NeST ndogo ndiyo sehemu kubwa ambako fedha za serikali imepelekwa kule kwa maana ya ujenzi wa shule, zahanati. Sasa kwenye implementation (utekelezaji) ya mfumo wa NeST ndogo kule wana njia moja tu ya ununuzi," anasema.

Anafafanua kuwa ununuzi una njia nyingi ambazo ni zaidi ya 16, lakini kwenye NeST ndogo wana njia moja tu ya kufanya ununuzi ambayo haiweki mfumo wa makundi hayo maalum.

"Sasa ile njia iliyoko kule ya wao kufanya manunuzi ina-limit categorization (inadhibiti). Hauwezi kutangaza tenda kuwa hii ni makundi maalum, hiyo limitation (mchanganuo) haina bali inafanya jumla tu…"

"Kwa hiyo kwa limitation yoyote ile inabidi uje uipate kwenye NeST kubwa lakini fedha nyingi za serikali inapelekwa kwenye NeST ndogo," anasema.

Kutokana na hilo, anasema wanashindwa kutangaza kazi ambazo walitakiwa wazitangaze kwa ajili ya makundi maalum kule kwenye NeST ndogo kwa sababu mfumo hauruhusu.

"Kwa nini nimekwambia hii changamoto na side effect (madhara) yake ni nini… kwanza ni kwa sababu kazi nyingi kuna baadhi ya makundi wamejisajili kwenye mfumo wa ujenzi, hawa hapa inakuwa ni vigumu kupata kazi kule kwenye mashule nk…"

"Kwa sababu mfumo hauwapendelei moja kwa moja na mfumo wa huku juu hatuwezi kuingilia kwani kule chini wana mfumo wao," anafafanua.

Inaendelea Uk. 17

# Giza nene utekelezaji...

Inatoka Uk. 16

"Sasa hii ni changamoto kubwa zinaathiri utekelezaji wa asilimia 30 kwa upande wa ujenzi,"anasema.

Anasema changamoto nyingine ni kasumba ya miaka ya nyuma ya kutoamini kuwa watu wa kawaida wanaweza kupata zabuni za serikali.

Anasema kwa sababu ni matakwa ya sheria kwamba zabuni zote zitangazwe kwenye NeST, hivyo watu wasipotumia mfumo huo hawawezi kupata zabuni hizo.

"Hata hapa umepishana na kijana kaja ana kampuni yake ananiambia nimsaidie kushinda tenda, sasa mimi sina namna ya kumsaidia kwa sababu kila kitu iko wazi kwenye NeST. Zabuni zinatangazwa wazi na wanaoshinda wanaonekana," anasema.

Anaeleza kuwa kwa Manispaa ya Ubungo, wamefanikiwa kutekeleza asilimia 50, huku asilimia 30 wakitekeleza kwenye maeneo ambayo ni usafi na ubebaji wa mizigo katika Stendi ya Mabasi ya Magufuli. "Tuna mitaa 90 katika hii mitaa 90 mpaka sasa tuna zaidi ya mitaa 30 ambazo zabuni zake wamepewa watu wa makundi maalum kwenye usafi…"

"Sehemu nyingine tuliyofanikiwa ni upande wa kubeba mizigo mfano pale Stendi ya Magufuli, tuna jumla ya vikundi saba na vyote vilivyopo pale ni vikundi maalum kwa maana tuna vikundi vinne vya vijana, viwili vya wanawake na tuna kikundi kimoja cha walemavu ambao wanaendelea kutoa huduma kupitia mfumo wa kundi maalum," anabainisha.

Anasema nje na makundi maalum kuna zabuni ambazo wanazitekeleza mfano ujenzi wa barabara ya Goba-Kinzudi kwa kiwango cha lami yenye kilomita moja…"

"Inatekelezwa na Kampuni ya Chiser, ni zaidi ya shilingi bilioni 1.4 inatumika na mmiliki ni mwanamke," anasema.

Anasema wamependelea vikundi vya kinamama katika huduma za utoaji wa chakula ambapo wana jumla ya vikundi 10.

Kuhusu kama wana utaratibu wa kutoa elimu, anasema mifumo yao haijawa rafiki sana na kwamba wana idara ya vijana chini ya idara ya maendeleo ya kijamii, ambapo wanakutana moja kwa moja kule mitaani.

**Mapendekezo**

Kutokana na hayo, anapendekeza yafanyike mabadiliko ili kuuwezesha mfumo wa NeST ndogo kuwa na upendeleo wa makundi maalum.

Pia aliwashauri vijana kufika Halmashauri kupata elimu kuhusiana na ununuzi wa umma na utoaji wa zabuni kabla hawajaunda vikundi.

"Mfano vijana wengine wanaunda kikundi kwa ajili ya kufyatua matofali ambapo mtaji ni mkubwa lakini badala yake wanatakiwa kuanzisha kikundi mfano kwa ajili ya kusafisha mitaro. Wawe wanakuja manispaa tutawasaidia kabla ya kuunda kikundi tutawashauri," anasema.




*Waumini wa Kanisa Katoliki la Mtakatifu Augustino Temboni, Dar es Salaam wakiwa kwenye foleni ya kupaka majivu Siku ya Jumatano ya Majivu kwa ajili ya Mfungo wa Kwaresma unaoendelea. (Na Mpigapicha Wetu).*

# BoT: Uchumi wa Tanzania unaimarika

Na Mwandishi WETU

TANZANIA imehitimisha mwaka 2025 ikiwa katika hali imara kiuchumi, hali inayotoa matumaini mazuri kwa mwaka huu wa 2026.

Taarifa ya Hali ya Uchumi ya Kila Mwezi (MER) inayochapishwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), inaonyesha kuwa uchumi umeimarika mwaka uliopita na viashiria vinaonyesha kuwa hali kama hiyo itaendelea mwaka huu.

Ripoti hiyo mpya, iliyotolewa Februari 18, 2026, inabainisha ukuaji thabiti wa uchumi, kudhibitiwa kwa mfumuko wa bei na kuimarika kwa biashara ya nje.

Mambo hayo yameiweka nchi katika nafasi nzuri licha ya mazingira magumu ya uchumi yanayotawala duniani hivi sasa.

MER ya Januari 2026 inaeleza kuwa Tanzania imehimili mwaka uliojaa sintofahamu za kimataifa, ikiwemo mabadiliko ya sera za biashara na misukosuko ya kijiografia.

Kimataifa, ukuaji wa uchumi ulizidi matarajio ya awali, huku Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) likirekebisha makadirio ya ukuaji wa uchumi wa dunia kwa mwaka 2025 hadi asilimia 3.3.

IMF inasema ukuaji huo utachochewa na matumizi binafsi na uwekezaji hasa katika eneo la teknolojia.

Kwa mujibu wa wachumi, kupungua kwa bei za bidhaa ghafi, hususan mafuta, kulisaidia kupunguza shinikizo la mfumuko wa bei duniani na hivyo kuziwezesha nchi nyingi, ikiwemo Tanzania, kuweza kufanya vizuri kiuchumi.



Gavana wa BoT, Emmanuel Tutuba

"Kwa kuzingatia kasi ya ukuaji iliyokuwa kubwa kuliko ilivyotarajiwa kuelekea mwishoni mwa mwaka 2025, Taarifa ya Mwonekano wa Uchumi wa Dunia (WEO) ya IMF ya Januari 2026 ilirekebisha ukuaji wa dunia kwa mwaka 2025 hadi asilimia 3.3 kutoka makadirio ya asilimia 3.2 yaliyotolewa Oktoba 2025, ikiashiria maboresho ya kiasi katika mtazamo wa muda mfupi," BoT inasema katika ripoti hiyo.

**Athari za uchumi wa dunia**

Kwa mujibu wa BoT, katika kutengeneza uchumi wake Tanzania ilinufaika na mazingira mazuri ya nje.

Mambo hayo ni kama vile kushuka kwa bei za mafuta ambako kulipunguza gharama za nishati na uzalishaji, huku bei nzuri ya dhahabu ikiongeza mapato ya mauzo ya nje, na hivyo kuimarisha urari wa biashara na kusaidia udhibiti wa mfumuko wa bei.

Kutokana na hali hiyo, BoT inaripoti kuwa uchumi uliendelea kushika kasi, ambapo Pato la Taifa halisi (GDP) lilikua kwa asilimia 6.4 katika robo ya tatu ya mwaka 2025, ukilinganisha na asilimia 6.1 katika kipindi kama hicho mwaka uliotangulia.

"Uchumi wa ndani uliendelea kuwa na kasi nzuri ya ukuaji katika robo ya tatu ya mwaka 2025, ukiungwa mkono na uwekezaji unaoendelea kutoka sekta ya umma na binafsi," MER mpya inaeleza.

Ripoti hiyo inabainisha kuwa kukua kwa Pato la Taifa kumechochewa na kilimo, madini na uchimbaji, ujenzi, huduma za kifedha na bima.

Katika hotuba ya mwisho wa mwaka aliyoitoa Desemba 2025, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aliutaja mwaka 2025 kuwa mwaka wa utendaji imara wa uchumi, huku GDP ya Tanzania ikikua kwa takribani asilimia 5.8 licha ya changamoto za ndani na nje ya nchi.

# Thamani ya dola yashitua Marekani

Na Mwandishi WETU

BENKI Kuu ya Marekani (BAC) imewataka wafanyabiashara, hasa wawekezaji kuwa makini na sarafu ya nchi hiyo; dola ambayo imeanza kutoa ishara za tahadhari kuhusu uimara wa thamani yake.

Kauli hiyo ya Benki Kuu ni moja ya dalili kuwa hata mkakati wa kisera unaweza usitatue tatizo la sarafu hiyo pindi litakapofikia hatua mbaya.

Benki hiyo imewataka wawekezaji na wafanyabiashara kuhakikisha kuwa wanafuatilia kwa karibu mwenendo wa uchumi hasa kuhusiana na thamani ya sarafu hiyo kwani zimeanza kuonekana kuporomoka kwa thamani yake katika mazingira yasiyotarajiwa.

Iwapo hilo litatokea, wanasema wachambuzi wa uchumi, kuna uwezekano wa wawekezaji kupoteza mali zao walizowekeza kwenye vitu visivyohamishika na hivyo kusababisha mtikisiko mkubwa kwenye uchumi.

BAC imetoa kauli hiyo baada ya baadhi ya wachambuzi kusema kuwa mwenendo wa dola wa hivi karibuni haupaswi kuleta wasi wasi kutokana na uimara wa uchumi wa Marekani.

Hata hivyo, BAC inasisitiza kuwa hali hiyo inaweza kubadilika na kuwataka wafanyabiashara, na hasa wawekezaji kuendelea kufuatilia mwenendo wa dola kwa karibu.

Hivi karibuni BAC ilichukua hatua kadhaa kutokana na kile ilichoeleza kuwa kushuka kwa dola kusiko kwa kawaida ambapo ilishuka kwa zaidi ya asilimia tano katika kipindi cha mwezi mmoja tu.

BAC inaonya kuwa hali kama hii ikiendelea inaweza kusababisha watu wengi kuanza kuuza dhamana zao kama njia ya kuepuka kushuka kwa thamani ya dhamana hizo na hivyo kusababisha soko la bidhaa kuzidiwa.

BAC ina wasi wasi kuwa inaweza kushindwa kutumia sera za fedha kudhibiti jambo kama hilo iwapo litatokea.

Katika kipindi cha wiki mbili zilizopita dola imekuwa ikionyesha tabia zisizotabirika. Kwanza ilishuka thamani katika kiwango ambacho hakijashuhudiwa katika kipindi cha miaka minne na kisha ghafla ikapanda baada ya Rais Trump kumteua Kevin Warsh kumrithi Jerome Powell kuwa Gavana wa Benki Kuu.


"Shuka-panda" hii ya dola tayari imeanza kuleta shaka kwenye biashara ya fedha na pia kwenye madini.

Wataalamu wengi wa uchumi nao wameanza kupatwa na mashaka kutokana na hali hiyo wakisema kuwa inavyoonyesha dola imeanza kuwa na tabia ambazo haziendani na misingi ya kiuchumi.

Kwa kawaida thamani ya sarafu ya nchi huimarika pale mapato ya nchi husika yanapopanda lakini Januari thamani ya dola ilishuka ingawa uchumi wa Marekani uliimarika zaidi ya Ulaya na Japan.

Hali hii imewafanya watalaamu wa biashara ya fedha na hisa nao kuanza kuingiwa na wasi wasi.

Hata hivyo, baadhi ya wachambuzi wanaamini kuwa thamani ya dola itatengemaa iwapo uchumi wa Marekani utaendelea kukua.



*Makamu Mwenyekiti wa CCM (Bara), Stephen Wasira, akisalimiana na Mama Maria Nyerere, mke wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere nyumbani kwake Msasani, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. (Picha na CCM)*

Habari

# Pengo kuzikwa kwenye kaburi alilojiandalia



Na Mwandishi WETU

KIFO cha Askofu Mkuu Mstaafu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo (pichani) kimeacha historia ya mtu aliyekuwa mchungaji mwaminifu, kiongozi mwenye busara na mtumishi aliyejitolea kwa dhati kujenga kanisa na taifa.

Kardinali Pengo alifariki Februari 19 jijini Dar es Salaam, alipokuwa akipatiwa matibabu katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) na tayari Rais Samia Suluhu Hassan ameshatoa salamu zake za rambirambi kufuatia kifo chake.

Kifo cha Kardinali Pengo kimetokea siku ya pili baada ya kuanza kwa kipindi cha mfungo wa Kwaresma.

Katika salamu zao, waumini wa Kanisa Katoliki nchini walizozitoa kupitia makundi mbalimbali kwenye mitandao ya kijamii, wanamwelezea Kardinali Pengo kama kiongozi wa kidini aliyejikita katika mafundisho ya kweli, aliyejitoa kujenga mshikamano wa waamini na kuyashika maadili ya Kikristo yaliyolenga haki, amani na upendo.

Kardinali Pengo alifahamika kwa tabia ya upole na kuzungumza taratibu hata pale alipozungumzia masuala nyeti na mazito ya kiimani au kuikosoa mifumo ya uongozi wa kisiasa, serikali na viongozi wake.

Katika nafasi yake ya uongozi wa kanisa alikuwa mstari wa mbele kuirekebisha serikali pale ilipokuwa ikifanya mambo tofauti na pia aliibeba imani katika kazi yake ya kichungaji kabla na baada ya kustaafu.

**Salamu za Rais**

Katika salamu zake za pole, Rais Samia amebainisha kuwa katika kipindi chote cha utumishi wake ndani ya Kanisa Katoliki, Kardinali Pengo alisimama imara kuhubiri amani, maadili na mshikamano wa kitaifa.

Ameeleza kuwa mchango wake mkubwa kwa taifa na kwa waumini wa Kanisa Katoliki utaendelea kukumbukwa na kuenziwa siku zote.

Naye Mwenyekiti Mstaafu wa Kanisa Katoliki Parokia ya Kijichi, John Choma amesema Kardinali Pengo ameacha alama kubwa isiyofutika kufanya vyema kazi yake ya kichungaji.

"Binafsi kama Mwenyekiti mstaafu nitamkumbuka sana. Kwa miaka sita ya Utume wangu Kijichi Mwadhama alitutembelea sana, alipenda sana kusali nasi hapa mara kwa mara…"

"Hata katika maandalizi yake ya Jubilei ya Miaka 50 ya Upadre wake sisi Kijichi tulikuwa wa kwanza kabisa Jimbo Kuu la Dar es Salaam kuambiwa wakati aliposhiriki nasi misa ya kufunga mwaka na mwaka uliofuata ndio mwezi wa sita ikawa Jubilei yake," amesema Choma.

Choma anakumbuka pia jinsi Kardinali Pengo alivyosali kanisani kwao wakati wa janga la Covid na yeye kuhangaika kujadiliana na Padre Massamba jinsi ya kuhakikisha usalama wake maana tayari alikuwa mzee.

**Kuzikwa Pugu**

Taratibu zilizotangazwa na Kanisa Katoliki Jimbo la Dar es Salaam zimeelezwa kuwa Kardinali Pengo atazikwa Jumamosi ijayo katika Kanisa la Hija, Pugu.

Hiyo ni kutokana na wosia aliouacha wakati akiwa hai alipoelekeza kuwa atakapofariki azikwe kwenye Kanisa hilo.

Kanisa la Hija Pugu lina umuhimu wa kipekee kwa Kanisa Katoliki nchini kwani inaaminika kuwa

Inaendelea Uk. 21

# Pengo kuzikwa...

Inatoka Uk. 20

ni kanisa la kwanza kujengwa wakati Ukatoliki ulipoingia nchini.

Pengo si tu alichagua eneo la kuzikwa bali pia aliratibu uchimbaji wa kaburi atakamozikwa. Kaburi hili lilichimbwa, kuandaliwa na kisha kuzibwa kusubiri mazishi yake.

Katika moja ya mahojiano na Kituo cha Televisheni cha Tumaini kinachomilikiwa na Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Pengo alisema eneo hilo alilipenda na kusisitiza kuwa ni matarajio yake kuwa uamuzi na chaguo lake hilo utaheshimiwa.

Hata hivyo, mara nyingi maaskofu, maaskofu wakuu na makadinali wa Kanisa Katoliki huzikwa ndani ya makanisa ya Kiaskofu (Cathedrals).

**Sababu za kuandaa kaburi**

Katika mahojiano yake na kituo kimoja cha habari Kardinali Pengo alisema ameandaa kuchagua azikwe Pugu kwa kuwa amehudumu katika kazi za Uaskofu Dar es Salaam kwa muda mrefu kuliko mahali pengine.

Pamoja na kuwa maaskofu huzikwa katika makanisa makubwa, lakini kanisa linatoa uhuru wa askofu kuchagua mahali pa kuzikwa.

Hilo ndilo lilimfanya Kardinali Pengo kuchagua kuzikwa katika Kanisa la Hija, mahali ambapo wamisionari wa kwanza kuja nchini nao walizikwa eneo hilo. Ingawa suala la kuchimba kaburi kabla hajafa liliwashitua watu wengi lakini Kardinali Pengo mwenyewe alisisitiza kuwa hata kama asingefanya hivyo ni dhahiri siku moja atakufa.

Hivyo akaona ni vema kufanya maandalizi kabla hajaitwa na Mungu.

Alisisitiza kuwa kuwepo au kutokuwepo kwa kaburi hakuzuii au kumwepusha mtu na kifo kwani Mungu ndiye anayepanga yote.

**Kadinali Pengo ni nani?**

Polycarp Kardinali Pengo alizaliwa Agosti 5, 1944 huko Sumbawanga mkoani Rukwa, eneo la nyanda za juu kusini lililo jirani na Ziwa Tanganyika.

Alikuwa ni mtoto wa sita katika familia ya watoto tisa.

Alionyesha wito wa kuwa padre tangu akiwa mdogo jambo ambalo lilimfanya dada yake mkubwa kuweka nadhiri ya kuhakikisha kuwa anamwendeleza mdogo wake hadi afikie azma yake hiyo.

Dada huyo, ambaye alikuwa wa kwanza kuzaliwa katika familia alifanya hivyo kwa kutumia kila alichopata kumwendeleza mdogo wake hadi azma yake ikatimia.

**Pengo alipata Daraja la Upadre mwaka 1971.**

Alisomea teolojia ya maadili huko Roma katika Chuo Kikuu cha Pontifical Lateran, ambako alipata Shahada ya Uzamivu (udaktari) mwaka 1977.

Alifundisha Teolojia ya Maadili katika Seminari Kuu ya Kipalapala iliyoko Tabora kwa muda mfupi, kisha akawa Gombera wa kwanza wa Seminari Kuu ya Segerea jijini Dar es Salaam hadi mwaka 1983.

Aliteuliwa kuwa Askofu wa Nachingwea (sasa Lindi) mwaka 1983, na baadaye Askofu mwanzilishi wa Jimbo la Tunduru–Masasi mwaka 1985.

Mwaka 1990 aliteuliwa kuwa Askofu Mwandamizi Dar es Salaam, akingojea kustaafu rasmi kwa Laurean Kardinali Rugambwa.

Mwaka 1992 akawa Askofu Mkuu wa Dar es Salaam kufuatia kustaafu kwa Kardinali Rugambwa ambaye alifariki dunia Desemba 1997.

Pengo alitangazwa kuwa Kardinali na Papa John Paul II katika mkutano wa makadinali (consistory) wa Februari 21, 1998.

Alikuwa miongoni mwa makardinali waliopiga kura katika mkutano wa kumchagua Papa mwaka 2005 uliomchagua Papa Benedict XVI na pia alishiriki kumchagua Papa Francis mwaka 2013.

Alikuwa mwanachama wa vyombo mbalimbali vya Curia ya Vatican, ikiwemo uinjilishaji wa mataifa, mafundisho ya imani, mazungumzo ya kidini na tamaduni (mabaraza), pamoja na Baraza Maalum la Afrika la Sinodi ya Maaskofu.

Tangu mwaka 2007 alikuwa rais wa SECAM (Shirikisho la Mabaraza ya Maaskofu Afrika na Madagascar). Septemba 18, 2012, aliteuliwa na Papa Benedict XVI kuwa mmoja wa wajumbe wa Sinodi kwa Mkutano Mkuu wa 13 wa kawaida wa Sinodi ya Maaskofu uliofanyika Oktoba 2012.

Papa Francis aliridhia ombi la Kardinali Pengo kustaafu uaskofu mkuu Agosti 15, 2019 na baadaye nafasi yake kuchukuliwa na Thaddaeus Ruwa'ichi, ambaye alikuwa mwanafunzi wake wakati akifundisha seminari.

Habari

# Rungu la msajili lashukia CUF




*Aliyekuwa Mwenyekiti wa CUF, Prof. Ibrahim Lipumba*

Na Mwandishi WETU

MAMBO ambayo Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania aliyafanya kwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) baada ya uchaguzi wake mwaka jana – 2025, amerudia kuyafanya kwa Chama cha Wananchi (CUF).

Kama ambavyo msajili alibatilisha baadhi ya viongozi walioteuliwa katika nafasi za Kamati Kuu, sasa msajili amebatilisha safu ya viongozi wa juu wa CUF waliochaguliwa katika uchaguzi uliofanyika mwaka juzi.

Hivi karibuni msajili alikiandikia barua CUF akibatilisha uchaguzi wa viongozi watatu wa ngazi za juu wa chama hicho kwa kile alichoeleza kuwa ukiukwaji wa Katiba ya chama kuhusiana na taratibu za uchaguzi wa ndani.

Mmoja wa viongozi ambaye msajili amesema hamtambui ni mwenyekiti wa taifa wa chama hicho, Profesa Ibrahim Lipumba ambaye alitangazwa mshindi kwenye uchaguzi uliofanyika 2024.

Baada ya uchaguzi wa Chadema mwishoni mwa mwaka jana, msajili alipokea malalamiko kutoka kwa mwanachama wa chama hicho na baada ya kupitia malalamiko hayo na utetezi kutoka kwa uongozi wa Chadema, msajili alibatilisha uteuzi wa wajumbe kadhaa wa Kamati Kuu akisema kuwa taratibu za uteuzi wa wajumbe hao hazikuzingatiwa.

**Sasa hali kama hiyo imetokea kwa CUF.**

Baada ya uchaguzi wa chama hicho mwaka 2024, msajili alipokea malalamiko kutoka kwa mwanachama wa CUF na baada ya kuyapitia pamoja na utetezi kutoka kwa chama hicho, msajili amebatilisha uchaguzi wa viongozi watatu wa ngazi za juu wa chama hicho.

Msajili anaeleza yaleyale kuwa kanuni za uchaguzi za chama hicho hazikuzingatiwa wakati wa uchaguzi.

Hata hivyo, Naibu Katibu Mkuu wa CUF (Bara), Magdalena Sakaya anapingana na uamuzi huo wa msajili akisema hakuna kanuni zilizokiukwa wakati wa uchaguzi wao.

Sakaya amesema chama kina vyombo vyake vya uamuzi, na iwapo msajili anaona uchaguzi wa mwenyekiti ulikuwa na dosari kwa kuwa kura hazikuzidi asilimia 50, basi hoja hiyo haina msingi.

Hatua hiyo ya msajili imezusha mpasuko katika chama hicho cha upinzani, yakiibuka makundi mawili.

Kundi moja bado linaamini kuwa viongozi hao waliochaguliwa bado ni halali licha ya hatua ya msajili kubatilisha uchaguzi wao huku kundi jingine likiwataka viongozi hao kuachia ngazi ili uchaguzi mwingine ufanyike.

**Msimamo wa msajili**

Msajili alibainisha kuwa Lipumba hakupata zaidi ya nusu ya kura zilizomchagua, jambo ambalo ni kinyume na kanuni inayotaka mshindi wa nafasi ya mwenyekiti apate zaidi ya nusu ya kura zote zilizopigwa.

Msajili amekitaka chama hicho kufanya uchaguzi mwingine ili kujaza nafasi hizo tatu za viongozi wa juu.

Inaendelea Uk. 23

# Rungu la msajili...

Inaendelea Uk. 22

Wiki iliyopita viongozi wanaomtambua Prof Lipumba na uongozi wake, waliitisha mkutano wa waandishi wa habari katika ofisi za makao makuu ya chama Buguruni jijini Dar es Salaam, ili kutoa ufafanuzi kuhusu sakata hilo.

Lakini mkutano huo ukageuka kuwa vurugu.

Wakati Sakaya akizungumza, kundi jingine la wanachama ambao wanaupinga uongozi uliopo madarakani lilifika na kuanza kufanya mkutano mwingine na waandishi wa habari nje ya ukumbi ambao Sakaya alikuwa anakutana na waandishi.

Hali hiyo ilisababisha mvutano na sintofahamu miongoni mwa waandishi na watu wengine.

Kundi hilo, ambalo lilimualika pia Msajili Msazidizi wa Vyama vya Siasa, Cisty Nyahoza, lilikuwa linalindwa na askari polisi.

Hali ilipozidi kuwa ngumu polisi walilazimika kuingilia kati na kuwakamata baadhi ya wanachama.

Akizungumza na vyombo vya habari baadaye, Nyahoza alisema siyo lazima uongozi wa CUF uitwe ofisini kwake kwenda kupewa maelekezo, bali msajili anaweza kuja kwenye ofisi za CUF kama alivyofanya yeye.

### Maswali juu ya maswali

Uamuzi huo wa msajili, ambao umekuja zaidi ya mwaka mmoja baada ya CUF kufanya uchaguzi wake umeibua maswali kutoka kwa watu mbalimbali.

Wengi wanajiuliza kwa nini imemchukua Msajili muda mrefu kulitolea uamuzi suala hilo wakati kwenye uchaguzi wa Chadema haikuchukua muda mrefu kiasi hicho?

Sasa ni dhahiri pia kuwa uamuzi huo umesababisha mvurugano na kudhoofisha umoja katika chama hicho cha upinzani.

Kwa kuwa hali kama hiyo ilikikumba pia chama kingine cha upinzani wadau wa demokrasia wameanza kuhoji lengo hasa la Msajili wa Vyama vya Siasa ni kuvilea vyama vya upinzani au kuvivuruga?

Uchambuzi uliofanywa unaonyesha kuwa mgogoro huu utazidi kukidhoofisha zaidi CUF ambacho kwa miaka ya hivi karibuni kimeshuhudia umaarufu wake ukiporomoka nchini.

> **"Wale watu si wanachama wa CUF. Waliitisha kikao bila ya uongozi kuwa na taarifa. Kama wangekuwa wanachama basi wangefuata taratibu..."**

Hata hivyo, kwa upande mwingine kuna watu wanahoji kuhusu demokrasia ndani ya vyama.

Wanasema kuwa haiwezekani kwa msajili kubatilisha uchaguzi wa ndani ya chama pasipo kuwepo kwa makosa ya dhahiri.

Wanasema wakati watu wakihoji hatua hiyo ya Msajili wanapaswa pia kuhoji iwapo kuna demokrasia ndani ya chama husika.

Uzoefu unaonyesha kuwa mgogoro huu wa sasa ndani ya CUF ulioibuliwa na Msajili utachukua muda mrefu kusuluhishwa iwapo Msajili mwenyewe hatochukua hatua za kukisaidia chama hicho kuondoa sintofahamu hiyo.

### CUF yamshitaki msajili

Akizungumza na Pambazuko mwishoni mwa wiki iliyopita, Sakaya, alisema tayari wamefungua kesi mahakamani kupinga uamuzi wa msajili huyo kutengua matokeo ya uchaguzi uliofanyika mwaka juzi ambao ulimuweka madarakani Profesa Ibrahim Lipumba na wenzake.

Akizungumzia vurugu zilizoibuka wiki iliyopita wakati akizungumza na waandishi wa habari, Sakaya amesema watu ambao waliitisha kikao kingine si wanachama wa chama chao.

"Wale watu si wanachama wa CUF. Waliitisha kikao bila ya uongozi kuwa na taarifa. Kama wangekuwa wanachama basi wangefuata taratibu za kuitisha kikao," anafafanua.

Alisema kikao hicho haramu ambacho kilikuwa kikilindwa na askari wa Jeshi Polisi wakiwa na magari matatu, ndicho ambacho kilitangaza kuuondoa madarakani uongozi halali wa CUF uliopo.

Wakati kikao hicho kinaendelea, Sakaya anasema, walikuwepo wanachama wao watatu ambao walikuwa wanapinga kilichokuwa kinaendelea lakini matokeo yake wakaishia kukamatwa na polisi.

Kilinge cha Mawasiliano



Na Loth MAKUZA

# Mizani ya PR Tanzania 2026

MIEZI michache iliyopita, nilipokuwa nikizungumza na wenzangu katika Mawasiliano na Umma (PR), swali moja lilikuwa likijirudia mara kwa mara, likiwa na msisitizo; je, tuko tayari kwa kile ambacho mwaka 2026 unaleta katika tasnia nchini Tanzania?

Siyo utayari wa kuwa na kaulimbiu pekee, bali kuitenda tasnia kwa vitendo.

Kwa mujibu wa tafiti kuhusu swali hilo ni takriban watalamu 600 wa PR waliulizwa namna mustakabali unavyoonekana kwa nchi zao.

Majibu hayakushangaza, kwamba kuna pengo kubwa. Viongozi wanaamini wafanyakazi wao wanaendana na kasi, ubunifu na wanabadilika haraka.

Watekelezaji wa hayo yasemwayo na wakubwa wao, wanafikiri tofauti. Wanasema wanafanya kazi kubwa huku wakiwa na timu ndogo. Uamuzi unacheleweshwa na ngazi za juu kutokana na ukiritimba.

Kwa mujibu wa Cision (Kampuni iliyofanya utafiti), asilimia 33 ya wakurugenzi wanaamini timu zao zinaendana na wakati, huku asilimia 14 tu ya wafanyakazi wanaokubaliana naye.

Lakini kuna ukweli ambao wengi hawataki kuusikia;

teknolojia haitaondoa fikra mbovu, kadiri matumizi ya akili unde (AI) inavyozidi kuwa na nguvu, rasilimali muhimu zaidi katika PR zinabaki kuwa za kibinadamu.

Waandishi wa habari bado watahitaji kufanya kazi na binadamu. Hadhira bado inaamini zaidi mchango mkubwa wa watu, badala yam ashine kufikisha taarifa.

Simulizi za kweli haziwezi kuhadithiwa na akili unde bila kupoteza uhalisia wake.

Ndiyo maana wataalamu wa PR wanapanga vipaumbele vyao kwa umakini. AI na 'automation' vinaongoza, lakini nyuma ya pazia kuna uhusiano na waandishi, ushirikiano na wabunifu, na mlingano mkali na mkakati wa kibiashara.

Huu siyo mgongano wa kimaslahi, bali ni mizani.

Zana za kiutendaji zinabadilika. Ufundi unaohitaji binadamu unabaki.

**Ujuzi wa kesho unaonekana wa jana**

Ukizungumzia ujuzi, kesho inaweza kukushangaza.

Simulizi na utengenezaji wa maudhui vinaongoza katika kufikia hadhira, huku uhusiano na vyombo vya habari vinafuatia kwa karibu.

Miaka ya karibuni, wataalamu wengi wa PR wamecheza na AI kwa udadisi. Wengine kwa hofu. Lakini 2026 itakuwa tofauti, huu ndio mwaka ambao majaribio yanaisha na nidhamu inaanza.

AI itatoka kuwa maajabu mapya na kuwa sehemu ya mchakato wa kazi. Kutoka kuwa kitu kinachosisimua kwenda hatua ya uwajibikaji zaidi.

Lakini mabadiliko makubwa zaidi yanatokea kimya kimya kwenye mawasiliano kipindi cha migogoro.

Hapa sasa, tasnia ya PR nchini Tanzania inaweza kuwa njia panda.

Timu lazima ziunganishe mikakati na utekelezaji. Menejimenti lazima ziondoe vizuizi badala ya kusherehekea na kufurahia mafanikio ya kuwepo AI.

AI hakika haitaweza kuchukua nafasi ya wataalamu wanaofanya majukumu ya PR, lakini itafichua tu udhaifu na kuwa chachu ya kuwainua wale wenye umakini kazini.

2026 ina chaguo moja kwa PR Tanzania, ambalo ni kubadilika na kufuata mabadiliko au kupuuza na kupotea kimya kimya.

Chaguo ni letu.

***Mwandishi wa safu hii ni mtaalamu wa Uhusiano na Umma (PR). Anapatikana kwa namba: 0625 704 995 na kupitia email; projects@lothmakuza.co.tz***

# ZEC yachoma nyaraka za uchaguzi

**Na Mwandishi WETU**

TUME ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) imeanza utekelezaji hatua ya kuteketeza nyaraka za Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 28 na 29, 2025 ambapo zoezi hilo limeanzia Kisiwa cha Pemba.

Taarifa za ZEC zinaeleza kuwa baadaye kazi hiyo itahamia katika kisiwa cha Unguja.

Mwenyekiti wa ZEC, Jaji George Kazi, amesema uteketezaji wa nyaraka hizo ni utekelezaji wa matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kifungu cha 98(3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar ya mwaka 2018.

Sheria hiyo inaipa ZEC mamlaka ya kuteketeza nyaraka za uchaguzi siku 90 baada ya kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu endapo hakutakuwa na katazo kutoka mahakamani.

ZEC imechukua hatua hiyo licha ya kuwepo kwa kesi kadhaa mahakamani zilizofunguliwa na chama cha ACT Wazalendo kupinga matokeo ya uchaguzi huo.

Ndio maana hatua hiyo ya kuharibu nyaraka imewashitua wadau wengi wa demokrasia wakihoji itakuwaje iwapo nyaraka hizo zitajhitajika baadaye mahakamani katika kesi hizo?

Aidha, wadau wengine wa demokrasia wanahoji kwa nini nyaraka muhimu kama hizo ziteketezwe haraka namna hiyo.

Kwa upande wake, chama cha ACT Wazalendo kimesema kimejipanga kuchukua hatua za kisheria ili kudai haki ya ushindi walioupata katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025.

Kauli hiyo imetolewa na Mnadhimu wa Kambi rasmi ya Upinzani katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Profesa Omar Fakih, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika Makao Makuu ya chama hicho eneo la Vuga, mjini Zanzibar.

Amesema katika uchaguzi huo, chama chao kilipata ushindi kwenye jumla ya majimbo 32 ya Ubunge, Uwakilishi na Udiwani, lakini wanadai matokeo hayo yaliporwa, hivyo watafuata taratibu za kisheria kudai haki yao.



**ZEC yajitetea**

Jaji Kazi ameeleza kuwa anatambua ya kuwa kuna kesi ambazo zinaendelea mahakamani kuhusu Uchaguzi Mkuu uliyofanyika Oktoba 2025 lakini hadi sasa bado tume yake haijapokea katazo lolote.

Alibainisha kuwa kabla ya kuteketeza nyaraka hizo ZEC ilijiridhisha kuwa hatua zote zinazowekwa kisheria zimezingatiwa.

Alisisitiza kuwa pamoja na kuwepo kwa kesi za uchaguzi mahakamani lakini ZEC haijapokea katazo lolote la kuharibu nyaraka hizo.

Hata hivyo, hakueleza kwa nini ZEC isifikirie kuwa kuwepo kwa kesi hizo kunaweza kuzifanya nyaraka hizo zihitajike kama vielelezo mahakamani.

Aidha, jaji huyo hakueleza kwa nini nyaraka hizo zimeteketezwa haraka namna hiyo.

Alisisitiza tu kuwa tume inalazimika kufuata utaratibu uliowekwa kisheria ambao unaitaka kuziharibu nyaraka hizo siku 90 baada ya uchaguzi kukamilika.

Kuteketezwa kwa nyaraka hizo kumefanyika chini ya uangalizi ili kuhakikisha kuwa linafanyika kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na sheria.

Kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi Zanzibar, shughuli hiyo ni sehemu ya shughuli zinazopaswa kufanyika baada ya kukamilika kwa uchaguzi mkuu.



# Tunakaribisha barua. Tuma kupitia

**Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba; +255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz**

## Mamlaka idhibiti foleni Barabara ya Morogoro

**Mhariri,**
MIONGONI mwa kero kubwa katika Jiji la Dar es Salaam ni foleni za magari barabarani hasa wakati huu ambao kuna marekebisho katika barabara nyingi ikiwemo ya Morogoro.

Mara nyingi nyakati za jioni au asubuhi unaweza kukaa kwenye foleni kwa zaidi ya saa mbili.

Ni zaidi ya miezi sita sasa tangu waanze kuchimbachimba hizi barabara na kibaya zaidi hawakamilishi sehemu moja bali wanarukia eneo lingine bila kukamilisha chochote.

Imefika hatua sasa hata hatuwaelewi wanachokifanya.

Kiukweli tumechoshwa na hii kero ya foleni inayosababishwa na marekebisho ya barabara. Tunaiomba mamlaka husika itusaidie kwa kukamilisha hizi barabara haraka.

**Janeth Shirima, Kimara, Dar es Salaam.**

## Nini kinaendelea Kituo cha Daladala Zingiziwa Chanika?

**Mhariri,**
NI miaka kadhaa sasa tangu mamlaka ilipoanza ujenzi wa Kituo cha Daladala cha Zingiziwa, Chanika, Dar es Salaam, lakini sasa kazi hiyo imetelekezwa.

Sisi wakazi wa Zingiziwa kwa kweli hatuelewi kinachoendelea, je ni fedha za umma zilizotumika zimepotea tu bure?

Kituo hiki kingekuwa ni msaada sana kwetu lakini sasa ni miaka inakimbia tu imekuwa ni kama wimbo.

Tungependa kupata majibu kutoka kwa mamlaka, nini kinaendelea?

**Juma Hashim**
**Chanika.**

## Tunalazimishwa kulipa 300/- wenye tiketi ya mitandaoni

**Mhariri,**
TUNAOMBA kufikisha kero yetu kwenye gazeti lako kuhusu walinzi wa Stendi ya Msamvu, Morogoro kwa tabia yao ya kutulazimisha kulipa shilingi 300 hata tukiwa na tiketi ya mtandaoni.

Lakini cha kushangaza wale wenye tiketi ya karatasi hawalipishwi shilingi 300 wanapoingia getini, sasa hatuelewi hii maana yake nini?

Mwenye tiketi ya mtandaoni na yule aliye na karatasi kuna tofauti gani? Tunaomba mamlaka itusaidie kwa hili maana huu ni uonevu.

**Rose Isaac**
**Ifakara, Morogoro.**

## Arusha tuwekewe taa za barabarani

**Mhariri,**
NAANDIKA kukupongeza kwa kazi nzuri unayoifanya Pamoja na waandishi wako. Hakika mnaelimisha, kutaarifu, kuonya na kupongeza panapostahili.

Pamoja na hilo, napenda kupitia gazeti lako kufikisha matamanio ya wananchi wengi wa Arusha – ya kuwepo kwa taa za barabarani.

Barabara nyingi za jiji hilo hazina taa, na zilizopo zimekaa kama mapambo kwa kuwa hazifanyi kazi. Hali ni mbaya sana kwenye mitaa, huko kunatisha kila kiza kinapoingia.

Kukosekana kwa mwanga kwenye Barabara zetu na mitaa, kunachochea kuwepo kwa vitendo vya uhalifu, kitu ambacho kinaharibu sifa nzuri ya Jiji la Arusha ambalo linajulikana duniani kwa kupokea wageni wengi kutoka nje ya Tanzania wanaokuja kutalii.

Naomba wahusika waliangalie hili, na kumhimiza mbunge wetu, Paul Makonda kulivalia njuga ili Arusha iwe jiji kwelikweli.

**Suleiman Macha,**
**Sakina, Arusha**



Na Rashid MTAGALUKA

Hoja Yangu

# Magari ya serikali kutumia gesi isiwe siasa

UAMUZI wa Naibu Waziri wa Nishati, Salome Makamba kukubali ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kisekta kuhusu magari ya serikali kuanza kutumia gesi asilia, badala ya mafuta ya petroli na dizeli, ni hatua inayostahili kupongezwa.

Waziri Makamba alisema hayo wiki iliyopita wakati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilipofanya ziara katika Kituo cha Gesi Iliyoshindiliwa (CNG), Mlimani, jijini Dar es Salaam, kwa kuzingatia faida kubwa ya kiuchumi

Kiukweli kama serikali itauweka uamuzi huu katika utekelezaji; ni ishara ya mabadiliko ya kimkakati katika namna taifa linavyoweza kusimamia matumizi ya fedha za umma kwa busara zaidi.

Kwa muda mrefu, serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kununua mafuta kwa ajili ya magari yake. Katika mazingira ambayo taifa linapambana kuongeza mapato ya ndani, kupunguza utegemezi wa mikopo, na kuelekeza rasilimali kwenye huduma za kijamii, kila shilingi inayookolewa ina thamani kubwa. Hivyo, wazo la kutumia gesi asilia (CNG) si tu la kiufundi, bali ni la kiuchumi na kimkakati.

Kupitia Tanzania Petroleum Development Corporation (TPDC), jitihada zimekuwa zikifanyika kusambaza miundombinu ya gesi katika maeneo mbalimbali ya nchi, hususan jijini Dar es Salaam. Hata hivyo, matumizi ya gesi katika sekta ya usafiri bado hayajafikia kiwango kinacholingana na uwezo tulionao.

Swali la msingi ni hili: kama tunayo rasilimali, kwa nini tusiipe kipaumbele katika matumizi ya ndani kabla ya kufikiria masoko ya nje? Magari ya serikali yanaweza kuwa sehemu nzuri ya kuanzia. Serikali ikiwa kinara wa matumizi ya gesi katika vyombo vyake, itatoa mfano kwa sekta binafsi na wananchi kwa ujumla.

Kwa mujibu wa tathmini mbalimbali, matumizi ya CNG yanaweza kupunguza gharama za mafuta kwa kiwango kikubwa. Ikiwa magari ya taasisi za umma kuanzia wizara, wakala, hadi halmashauri yataanza kutumia gesi, mabilioni ya shilingi yanaweza kuokolewa kila mwaka.

Fedha hizo zinaweza kuelekezwa katika miradi ya maendeleo, kulipa madeni ya ndani, au kuboresha maslahi ya watumishi wa umma.

Lakini pamoja na nia njema, utekelezaji wake utahitaji umakini. Kwanza, lazima kuwepo na mpango wa kitaifa wa kubadilisha magari au kuyawezesha kutumia mifumo ya gesi.

Pili, miundombinu ya vituo vya kujazia gesi iongezwe kwa kasi ili kuepusha usumbufu kwa watumiaji.

Tatu, lazima kuwe na kanuni na mwongozo wa wazi utakaosimamia mabadiliko hayo, ili yasigeuke kuwa mradi wa majaribio usio na matokeo.

Zaidi ya faida za kiuchumi, gesi ni nishati safi ikilinganishwa na mafuta.

Hivyo, hatua hii inaweza kusaidia kupunguza uchafuzi wa hewa mijini na kuchangia katika jitihada za kimataifa za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Tanzania inaweza kujijengea taswira ya taifa linalotumia rasilimali zake kwa njia endelevu na rafiki kwa mazingira, ikiwa hayo yatafanyika.

Kwa mtazamo wangu, kukubaliwa kwa ushauri wa Kamati ya Bunge ni mwanzo mzuri. Hata hivyo, mafanikio yake yatapimwa si kwa kauli, bali kwa utekelezaji.

Serikali inapaswa kuweka ratiba mahsusi, malengo yanayopimika, na uwazi katika utekelezaji wake.

***Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com***



Makala

# Dawasa na mapinduzi ya huduma kimtandao

Na Mwandishi WETU

KATIKA hatua ya kuendana na kasi ya mageuzi ya teknolojia, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (Dawasa), imeanzisha mfumo wa kidijitali unaowawezesha wakazi wa Dar es Salaam kujisajili kuomba kuunganishiwa huduma ya maji kwa njia ya mtandao.

Mfumo huu ni suluhisho la kisasa linalolenga kurahisisha taratibu, kupunguza foleni na kuongeza uwazi katika utoaji huduma.

Kwa muda mrefu, maombi ya kuunganishiwa maji yalihitaji mteja kufika ofisini, kujaza fomu kwa mkono na kusubiri uthibitisho kwa muda mrefu.




Kupitia mfumo huu mpya, mteja anaweza kutuma maombi akiwa nyumbani au kazini kwa kutumia simu janja au kompyuta yenye intaneti.

Hii inaokoa muda na gharama za usafiri, huku ikiimarisha ufanisi wa taasisi.

Hatua ya kwanza ni kutembelea tovuti rasmi ya Dawasa na kufungua akaunti kwa kubonyeza sehemu ya "Jisajili." Mteja huingiza taarifa zake muhimu ikiwamo jina kamili, namba ya simu, barua pepe na namba ya kitambulisho.

Baada ya kuthibitisha usajili kupitia ujumbe wa simu au barua pepe, mteja anaingia kwenye akaunti yake na kujaza fomu ya maombi ya kuunganishiwa maji.

Katika fomu hiyo, mteja huweka anwani kamili ya makazi au biashara, aina ya jengo na kupakia nyaraka zinazohitajika kama nakala ya kitambulisho au uthibitisho wa umiliki wa eneo.

Baada ya kuhakiki taarifa, maombi hutumwa na mteja hupokea namba ya kumbukumbu kwa ajili ya kufuatilia hatua zinazofuata.

Mfumo huu pia unamwezesha mteja kuona maendeleo ya maombi yake – kuanzia kupokelewa kwa maombi, kupanga ukaguzi wa eneo hadi kutumiwa taarifa ya gharama za kuunganishiwa.

Malipo yanaweza kufanyika kwa njia za kidijitali kama vile mitandao ya simu au benki, jambo linalorahisisha zaidi mchakato mzima.

Kwa kuanzisha mfumo huu, Dawasa imeonyesha dhamira ya kuboresha huduma kwa kutumia teknolojia.

Ni hatua inayoongeza uwazi, inapunguza urasimu na kuweka mwananchi katikati ya utoaji huduma. Mfumo huu siyo tu umeleta urahisi, bali pia umeweka msingi wa huduma za maji zinazokwenda sambamba na mahitaji ya jiji linalokua kwa kasi kama Dar es Salaam.

Kutokana na hatua hii muhimu inayoendana na kasi ya mabadiliko ya kuhudumia wananchi, Dawasa inapaswa kuhakikisha mfumo huu unafanya kazi muda wote na pengine kufikiria kuweka mfumo utakaomuwezesha mteja kujaza fomu bila kulazimika kuwa na intaneti.

# Habari katika picha

*Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Mwinyi washiriki futari na makundi mbalimbali ya wananchi katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, Ikulu ya Tunguu, Zanzibar juzi. (Picha na Ikulu).*










*Lundo la taka likielekea kuziba Barabara ya Malamba Mawili-Makuti kutokana na mamlaka zinahusika na usafi kushindwa kuziondoa kwa wakati na kusababisha kero kwa watumiaji wa barabara hiyo, Jijini Dar es Salaam juzi. (Na Mpigapicha Wetu)*



Na Anti MSHAURI

# Nidhamu kwenye biashara itakusaidia




HABARI msomaji wangu wa safu ya uhusiano. Kama ilivyo ada, nakukaribisha uweze kufahamu mengi juu ya maisha.

Mada ya wiki hii inahusu mambo muhimu ya kuzingatia unapokuwa unafanya au unatamani kuanza biashara.

Ili uweze kufanikiwa kwenye biashara, unapaswa kujikita katika malengo mahsusi uliyojiwekea kwani hayo ndiyo yatakusaidia kusonga mbele.

Mambo ya kuzingatia ni pamoja na malengo ya biashara uliyojiwekea na kuyafanyia kazi, simamia fedha kwa ufanisi na epuka matumizi yasiyo ya lazima.

Jingine ni kuzingatia wateja. Hapa unapaswa kutoa huduma bora kwa wateja wako na kamwe usiwakwaze kwa mambo madogo madogo ya kukosa chenji hasa ndogo kama shilingi mia, hamsini na nyingine vinginevyo mambo hayo yakizidi utawakimbiza hivyo malengo yako hayatafika unapotaka.

Lakini pia unapaswa kuwa na nidhamu katika biashara yako inaweza kukusaidia hivyo unapaswa kuongeza uaminifu kwa wateja wako, kuboresha sifa za biashara ufanyayo na njia nyingine.

Pia kuona thamani kwa pato la biashara yako. Hapa unapaswa kuwa mwangalifu katika matumizi na epuka matumizi yasiyo na tija.

Kama biashara yako uliianzisha kwa kutumia mkopo, ilikupasa awali kufanya tathimini kama aina hiyo ya biashara itaingiza kipato ambacho kitakuwezesha kuulipa mkopo huo kwa wakati.

Wakati unaendesha biashara ambayo mtaji wake umetokana na mkopo unapaswa kuwa na nidhamu sana katika hesabu za biashara na kuhakikisha kuwa mkopo unalipwa kama ulivyokubaliana na aliyekukopesha.

Tukutane wiki ijayo.

***Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.***

# Mavazi ya stara yanayobamba



TUKO kwenye mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan na Kwaresma, ambao unatumika kwa kufunga na kujitakasa ili kujiweka karibu na Mungu.

Kwa namna ya kipekee, Waislamu wanatakiwa kuvaa mavazi ya kujistiri hususani kufunika kichwa.

Kutokana na hilo, mtindo unaotamba kwa sasa ni nguo za stara aina ya Abaya, Kaftan, suti star na nyingine nyingi kulingana na uhitaji wa mhusika.

Abaya nzuri zinaweza kuanzia shilingi 150,000 huku aina nyingine ya nguo za stara za mfungo wa mwezi huu ambazo ni kitambaa cha satini zikianzia 30,000 madukani.

Yapo pia mavazi ambayo yameshonwa vyema kwa vitambaa vya kung'aa na kupiticha ukosi wa rangi tofauti na kitambaa husika ili kukipendezesha zaidi.

Unaweza pia kuvaa baibui vazi lililozoeleka ama kuvaa gauni la kawaida refu lenye kumwaga na kukufanya nawe uwe nadhifu katika msimu huu wa mfungo Mtakatifu.

Mavazi haya huvaliwa pamoja na mitandio ambayo hufungwa kwa kufunika kichwa kwa kurushia mabegani ama kuzungusha kichwani.

Vaa mavazi haya na kuongeza urembo kama pochi inayoendana na mavazi.



# Fanya ngozi ya uso kuwa softi

NGOZI ya usoni inavutia kutokana na matunzo haswa kwa kufuata ratiba bora kuanzia namna ya kuosha hadi vitu unavyovitumia.

Hapa nimekuwekea vitu vingine vya kubusti mwonekano wako kama ifuatavyo;

*Tumia mafuta ya vaseline ya mgando kijiko kimoja na kiini cha yai.

Osha vizuri uso wako kisha kausha vizuri.

Changanya mafuta na kiini cha yai koroga vyema na upake usoni kwa kujimasage, kaa na mchanganyiko usoni kwa dakika 30, kisha nawa kwa maji safi ya uvuguvugu usitumie sabuni.

Fanya hivi mara mbili kwa wiki na utaona matok





# Nameless ampa heshima ya ufalme Marioo

Na Mwandishi WETU

MSANII mkongwe kutoka Kenya, Nameless, ameonyesha heshima na upendo kwa msanii wa Bongo Fleva kutoka Tanzania, Marioo baada ya kushirikiana kwenye wimbo wa “Nasinzia II.”

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Nameless aliandika kuwa amefurahia kufanya remix hiyo huku akimtaja Marioo kama “brother wangu wa Tanzania”, akisisitiza kuwa ameleta vibe mpya inayopendwa zaidi na kizazi cha sasa.

“Nilifurahi sana kufanya hii remix na brother kutoka Tanzania, Marioo… ameubariki wimbo huu kwa vibe mpya ambayo inapendwa sana younger generation…”

“Marioo uko na heshima yangu! Halafu uko na team ya nguvu! Hapo sawa King!!! Tuzidiii!!” aliandika Nameless.

Nameless pia aliishukuru Afrika Mashariki kwa sapoti waliyompa kwa miaka mingi.

# Trump amfagilia Nicki Minaj

Na Mwandishi WETU

KATIKA hali isiyo ya kawaida Rais wa Marekani, Donald Trump ameonyesha hisia zake hadharani kumsifia msanii wa hip hop, Nicki Minaj.

Tukio hilo lilitokea wakati wa mapokezi ya Black History Month (mwezi wa historia ya watu weusi) yaliyofanyika Ikulu ya Marekani hivi karibuni.

Rais Trump alitumia jukwaa hilo kumtambua na kumsifia rapa huyo ambaye kwa sasa anaonekana kuwa mshirika wake mkuu wa kisiasa.




# Jinsi ya kusoma Pambazuko





# Yanga joto, Simba kitete





Na Mwandishi WETU

JOTO la dabi ya watani wa jadi; Simba SC na Yanga SC, limezidi kupanda, ingawa sasa kimuhemuhe kimehamia kwa wasemaji wa vilabu hivi viwili vikubwa Tanzania.

Ni wazi hakuna mechi kubwa na yenye msisimko inayosubiriwa kwa hamu kila msimu isipokuwa ni Simba 'Mnyama' dhidi ya Yanga - Wana Jangwani hii ndio mechi kubwa na yenye kukonga nyoyo za mashabiki wengi ndani na hata nje ya Tanzania.

Kila msemaji ameonekana kuvutia upande wake na safari hii akionyesha kumshona mpinzani wake, Msemaji wa Simba, Ahmed Ally amesema; "tumejipanga vizuri safari hii, tutamfunga Yanga hata mechi wapeleke Afrika Kusini, kokote kule tunacheza naye kwani timu tunayo."

Kwa upande wake Msemaji wa Yanga, Ally Kamwe alisema "Wao si walitucheka tulivyoshindwa kufuzu Klabu Bingwa Afrika, sasa watatueleza sisi ni kina nani, nakuambiaje tarehe 1 ndio watatujua sisi kina nani tunamshona mtu vizuri kabisa."

Wiki iliyopita Klabu ya Simba waliandika barua kwenda kwa bodi ya ligi wakiomba ufafanuzi kuhusu mchezo huo wa dabi kupelekwa Zanzibar katika Dimba la Amani na siyo Benjamini Mkapa, Dar es Salaam kama ilivyopangwa hapo awali.

Hata Hivyo, bodi hiyo waliwajibu kuwa Yanga ndiyo wenyeji wa mchezo, hivyo wanabeba uamuzi wa kupeleka mchezo katika kiwanja chochote ambacho kimeaainishwa na Yanga kama uwanja wao nyumbani.

Sasa ni rasmi mchezo huo utachezwa Machi 1, 2026 - siku ya Jumapili na ikumbukwe katika michezo mitano ya mwisho iliyowakutanisha watani hao, Simba ameambulia kichapo mara zote.

Sasa swali linakuja, je, safari hii Simba wataweza kujinasua kwa kichapo cha watani wao Yanga au ndio vipigo vitaendelea?

*GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION